**28 JUNI, 2022**

**BUNGE LA TANZANIA**

___________

# MAJADILIANO YA BUNGE

___________

## MKUTANO WA SABA

## Kikao cha Hamsini na Tatu – Tarehe 28 Juni, 2022

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Katibu!

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Maswali Waheshimiwa Wabunge tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguruka, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 464

**Serikali kujenga kingo za Mto Kanoni**

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga kingo za Mto Kanoni unaopita katikati ya Mji wa Bukoba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguruka, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashaurii ya Manispaa ya Bukoba mwezi Februari, 2022 ilitumia shilingi milioni sita kupitia mapato ya ndani kwa ajili ya kusafisha, kupanua na kuongeza kina cha Mto Kanoni.

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa changamoto hiyo Serikali katika mwaka wa fedha 2022/2023 imejumuisha mradi wa ujenzi wa kingo za Mto Kanoni kwenye Mpango wa *TACTIC* Awamu ya Pili unaotarajiwa kuanza mwezi Januari, 2023, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguruka, swali la nyongeza.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nina swali moja la nyongeza.

Je, wakati huo ambao taratibu za kujenga kingo zinaendelea, Serikali haioni haja ya kutoa fedha angalau Shilingi milioni 100 kwa ajili ya kusafisha Mto Kanoni ili kupunguza athari zake hususan Kata nne ambazo zinaathirika zaidi; Kata ya Bilele, Bakoba, Hamugembe na Nshambya? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):**

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguruka, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Oliver Semuguruka kwa kadri anavyowakilisha wananchi wa Mkoa wa Kagera, lakini pia, anavyowasemea ipasavyo wananchi wa Mkoa huo. Vile vile nampongeza sana Mheshimiwa Stephen Byabato, Mbunge wa Jimbo la Bukoba Mjini anavyowasemea na kuwawakilisha ipasavyo wananchi wa Bukoba na anavyoshirikiana na Waheshimiwa Wabunge wa Viti Maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitambue kwamba wapo Waheshimiwa Madiwani, Mstahiki Meya na Mkurugenzi wa Bukoba Manispaa. Nitoe maelekezo kwa Mkurugenzi kuhakikisha wakati tunasubiri mradi huu wa ujenzi wa kingo kwa maana ya mradi wa *TACTIC,* watenge fedha kwa kadri inavyowezekana kuendelea kuboresha kingo na kina za Mto Kanoni ili kuzuia madhara hayo wakati bajeti hiyo inakuja kutekelezwa, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Afya Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota Mbunge wa Nanyamba, sasa aulize swali lake.

Na. 465

**Hitaji la watumishi Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini**

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka Watumishi wa kutosha katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini iliyopo Mtwara?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mtwara ilizinduliwa mwezi Oktoba, 2021 ikiwa na watumishi 45. Kwenye kibali cha sasa cha ajira imepangiwa watumishi wapya 112 itakayofanya idadi ya watumishi kufikia 157 mwezi Julai, 2022, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa sababu matarajio ya Hospitali ile ya Rufaa ni kutoa huduma za kibingwa, lakini kwa sasa tuna Daktari Bingwa mmoja tu; na katika jibu la msingi amesema kwamba anasubiri ajira mpya; je, ni lini Serikali italeta Madaktari Bingwa ili huduma za kibingwa zianze kutolewa katika hospitali hiyo?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, ni kwamba, ili wataalam hao waweze kufanya kazi kwa ufanisi, wanahitaji vifaa. Tunashukuru Serikali kwa kutuletea fedha za ununuzi za *MRI* na *CT-Scan,* lakini kwa sababu hawana Bodi ya Manunuzi, vifaa hivyo vimeagizwa kupitia *Ocean Road*; je, ni lini vifaa hivyo vitapatikana katika hospitali yetu ya Rufaa ya Kanda ya Kusini Mtwara? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Abdallah Chikota, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja la kwanza kuhusu *ma-Specialist,* inapofikia mwezi Julai mwaka huu 2022, kwa sababu tayari ma-*specialist* wawili wako pale na kwenye kibali hiki wako ma-*specialist* wanane, kwa hiyo, hospitali hiyo itakuwa na ma-*specialist* 10.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili ni kuhusu vifaa tiba. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, vifaa hivyo viko kwenye manunuzi, na tayari viko kwa ajili ya kuja nchini mpaka Oktoba vitakuwa vimefungwa na kazi itakuwa imeanza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Charles Kajege, swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Katika mgao wa watumishi wa afya ambao umefanyika juzi, nimeona bado katika vituo vyangu vya afya vya Kasaunga, Kisorya na Kasuguti havikupata; je, nini kauli ya Serikali sasa kuhusiana na upungufu huo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, labda nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba aliona Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI akisema kuna nafasi zaidi ya 700 ambazo bado hazijapata watu, lakini kwenye Wizara ya Afya kuna nafasi vilevile ambazo zinaweza zikabaki. Watashirikiana Waziri wa Afya na Waziri wa TAMISEMI kuona, na aje tupange ili tuone ni namna gani inaweza kufanyika *ku-fill* hizo *gap* anazozisema. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna Mtanda, swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi. Nami naomba niulize swali moja.

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya watumishi wa afya wanaohitajika katika Halmashauri ya Wilaya ya Newala ni 624, waliopo mpaka sasa ni 119 sawa na asilimia 19, na tuliopata juzi ni 38 tu, upungufu bado upo; je, Serikali inasema nini kuhusu kujaza nafasi za watumishi katika kada ya afya kwa Halmashauri ya Jimbo la Newala Vijijini? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ninachoweza kumwambia Mheshimiwa Mbunge ni kwamba, jinsi ambavyo bajeti itaendelea kuruhusu, maeneo kama hayo ambayo anayasema Mheshimiwa Mbunge yataendelea kupewa kipaumbele. Utaona wakati wa *application* wa hizi nafasi zilizotangazwa, umeona kabisa yameainishwa maeneo ambayo wanaruhusiwa watumishi *ku-apply* na wametajiwa kabisa utaenda hapa, utaenda hapa. Tutaendelea kusisitiza kabisa maeneo yenye upungufu zaidi yanapotokea kibali ndiyo yapewe kipaumbele. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Jimbo la Tabora Mjini lina Hospitali ya Rufaa ya Kitete. Hospitali hii ina upungufu wa Madaktari Bingwa wasiopungua tisa na ni ahadi ya muda mrefu Serikali kutuongezea

Madaktari Bingwa. Sijui Serikali itatuletea lini hao Madaktari Bingwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna shida ya Madaktari bingwa; japo wapo, lakini hawatoshi. Niendelee kumwomba Mheshimiwa Mbunge tushirikiane mimi na yeye kwa sababu kuna ambao wako shuleni sasa hivi, tena wengine wanatokea pale Kitete. Vile vile jinsi ambavyo wanamaliza tuendelee kuwapangia na kwa sababu sijaiangalia Kitete *specifically,* tutaangalia kwenye mgao huu kama kuna kilichofanyika kwenye eneo la Kitete.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, swali la nyongeza.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Ni lini Serikali itaongeza wafanyakazi kwa maana ya Matabibu katika Kituo cha Afya cha Matemanga, Nakapanya na Mtakanini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, maeneo aliyotaja Mheshimiwa Mbunge ni mojawapo ya maeneo ambayo hata sisi tunajua yana watumishi wachache na ni maeneo ambayo wengi wakipangiwa wanahama. Namwomba Mheshimiwa Mbunge kama ambavyo nilimjibu Mheshimiwa Mbunge mwenzake, kwenye nafasi ambazo ametangaza Waziri wa TAMISEMI ametaja, tukutane tuangalie na sisi upande wa Afya tuweze kuona namna ya kutoa kipaumbele kwa maeneo hayo kwenye hizi nafasi ambazo zilipungua.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Halmashauri ya Mji wa Bunda ina mahitaji ya watumishi wa afya wakiwepo Madaktari na Manesi 402. Waliopo ni 184, mahitaji ni 218: Je, katika hizo ajira mpya katika mgao wa nchi nzima, Halmashauri ya Mji wa Bunda ni sehemu mojawapo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naweza kumwambia ni sehemu mojawapo ambayo inafikiriwa kupangiwa, lakini wala asiogope kwa sababu inapokwenda kuwa Hospitali ya Nyerere, ile ya Kanda ambayo inajengwa Mara nayo ni sehemu mojawapo ambayo itakwenda kupunguza mahitaji ya watumishi kwenye eneo hilo la mkoa wao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata, swali la nyongeza.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa napenda kuishukuru Serikali kwa kutuletea vifaa tiba katika Hospitali ya Rufaa Mkoani Rukwa; je, ni lini sasa Serikali itatuletea Daktari Bingwa wa mifupa? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, nadhani swali la Mheshimiwa Mbunge ni *specific*. Naomba tuje tuangalie kama eneo, kuona kama Mkoa huo hauna kabisa Daktari wa mifupa, tukae na Mheshimiwa ili tuhakikishe kabla ya mwezi wa Oktoba amepatikana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Jonathan Msambatavangu, Mbunge wa Iringa Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 466

**Ombi la Kubadilisha Hospitali ya Mkoa na Wilaya – Iringa**

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU** aliuliza:-

Je, ni lini ombi la kubadilishana Hospitali ya Mkoa na ya Wilaya litafanyiwa kazi kuruhusu upanuzi wa Hospitali ya Mkoa wa Iringa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, Mbunge wa Iringa Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imepokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge, hivyo mwezi Julai 2022 timu ya wataalamu itakwenda Mkoani Iringa ili kuja na ushauri wa kitaalamu wa namna ya kutekeleza suala hili bila kuathiri mfumo wa utoaji wa huduma za afya katika Mkoa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, swali la nyongeza.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza naishukuru Serikali kwa majibu mazuri ambayo wametupatia, nami nakubaliana nayo na wala hatuna shida kwenye majibu hayo, isipokuwa tu, tutakapokuja kujadiliana nafikiri tunaweza tukafikia muafaka.

Mheshimiwa Spika, kwanza tunawashukuru kwa watumishi mliotuletea 26 ndani ya Manispaa ya Iringa wanaokwenda kwenye zahanati zetu na vituo vya afya na kwa ajili ya ujenzi wa wodi pale Frelimo. Ili kupunguza

changamoto ya hiyo Hospitali ya Mkoa, Serikali ina mpango gani sasa wa kutujengea wodi ya watoto katika Hospitali ya Frelimo na wodi ile ya *Internal Medicine* kwa ajili ya wagonjwa wa kawaida katika Hospitali ya Frelimo pamoja na kututengenezea zile *rooms* za *reproductive health pharmacy* na *CT* katika Hospitali ya Frelimo ili kupunguza changamoto ya Hospitali ya Mkoa wa Iringa?

Mheshimiwa Spika, pia ule mgao tulioomba kwa Hospitali ya Mkoa wa Iringa; je, tumepata Madaktari? Maana tulikuwa tuna upungufu wa watumishi karibu 200; ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwenye suala lake la kwanza la ujenzi wa wodi ya akina mama na Watoto, kama ambavyo Waziri wa Afya Mheshimiwa Ummy Mwalimu alisema, katika ununuzi wa vifaa na manunuzi yote ambayo yamefanyika kwa ajili ya vitu mbalimbali kwenye fedha ambazo Rais wetu alitupa, shilingi trilioni 1.3, imeokolewa shilingi bilioni 13, kwa maana tumenunua kwa bei rahisi zaidi kuliko ilivyotegemewa.

Mheshimiwa Spika, sisi na Mheshimiwa Mbunge kama ambavyo tumezoea kukaa pamoja, tunaweza tukakaa tuone kipaumbele tushirikiane na Waziri wa TAMISEMI ili anachokisema kiweze kufanyika.

Mheshimiwa Spika, suala lako la pili linazungumzia masuala ya Hospitali yake ya Mkoa. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, wakati tunakuja na ile timu, mimi naye tutakuwa pamoja na nina uhakika kwamba anachokifikiria kitakwenda kutekelezwa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Mkundi, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwa kuwa Serikali ilikubali ombi la kupandisha hadhi Hospitali ya Wilaya ya Ukerewe ya Nansio kuwa na hadhi ya Rufaa ya Mkoa, na tayari imetoa fedha fedha Shilingi bilioni tatu na ujenzi umeanza, lakini kuna sintofahamu kubwa inayosababisha wananchi wa Ukerewe kuwa na hofu kama matarajio yao yatafikiwa na thamani ya fedha ile kweli itafikiwa: Nataka kupata kauli ya Serikali, mnasemaje juu ya hili kuhakikisha kwamba matarajio ya wananchi wa Ukerewe na thamani ya fedha ile kweli inapatikana? Nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo Mbunge anakumbuka yeye mwenyewe alifika Wizarani, tukakaa mimi na yeye na Mheshimiwa Waziri wa Afya. Mheshimiwa Waziri wa Afya ameshaunda timu imekwenda Ukerewe kwa ajili ya kuangalia kitaalam ni nini hasa kinaleta sintofahamu hasa kwenye mahesabu. Pia ameshanielekeza, mimi na yeye tutakwenda, nitamchukua yeye twende pamoja baada ya kuchukua ile ripoti ya kitaalam tujadili na Baraza la Madiwani na wataalam ili tufikie muafaka ambao utafanya shughuli zilizoko pale ziweze kuendelea.

Mheshimiwa Spika, vilevile tayari wameongezewa zaidi ya Shilingi bilioni tatu kwa ajili ya kujenga yale maghorofa ambayo walitamani yajengwe eneo lile.

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa Kata ya Masama Kati tayari tulishatenga eneo kwa maana ya Kituo cha Afya chenye hadhi ya Kituo cha Afya na wewe mwenyewe umeshafika

pale, na tayari tumeshatenga fedha ya kujenga *OPD*: Je, ni lini Serikali itatuletea fedha ya kumalizia majengo hayo yaliyobaki ambayo pia ni ahadi yako kama sehemu ya Serikali?

**SPIKA:** Hilo swali ni la TAMISEMI, Naibu Waziri TAMISEMI msaidie kumjibu Mheshimiwa Mbunge swali lake, siyo swali la Wizara ya Afya.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, Mbunge wa Jimbo la Hai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nipokee ombi la Mheshimiwa Saashisha Mafuwe. Nafahamu tulishafanya ziara kule pia, tukaenda kwa Nsila, tumeanza ujenzi wa Kituo cha Afya kwa Shilingi milioni 250, nafikiri zinaongezeka nyingine. Hicho tutaenda kukifanyia tathmini kuona kama kinakidhi vigezo vya kujenga Kituo cha Afya tuweze kupeleka fedha kwa awamu, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Dkt. Dugange ahsante sana kwa majibu yako kwa swali ambalo lilikuwa halikuhusu wewe. Ahsante sana tunakushukuru. *(Makofi)*

Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Nkasi Kaskazini, sasa aulize swali lake.

Na. 467

**Kupitia upya mipaka ya hifadhi na makazi Nkasi**

**MHE. AIDA J. KHENANI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupitia upya mipaka ya hifadhi na makazi ya wananchi Wilayani Nkasi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Nkasi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza kutatua changamoto hiyo kwa kuweka vigingi ambapo hadi sasa jumla ya vigingi 111 vimewekwa kati ya vigingi 322 vinavyohitajika. Zoezi hili linaendelea hata kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ambapo vigingi vilivyobaki vitawekwa. Serikali itaendelea na jitihada za kutoa elimu kwa wananchi kuhusu namna ya kutambua na kuheshimu mipaka ya hifadhi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, pamoja na majibu ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; mipaka hii ambayo inazungumzwa leo iliwekwa mwaka 1948. Ukiangalia idadi ya watu ilikuwa ni watu wachache kuliko ilivyo leo. Kwa kuwa hii migogoro imekuwa ya muda mrefu na ilisababisha tamko na

maagizo ya Waziri Mkuu hapa Bungeni kwa Wizara ya Maliasili na Utalii kuja Nkansi kupitia upya mipaka hiyo kwa kushirikiana na TAMISEMI, mpaka leo hamjafika. Ni lini mtatekeleza agizo la Waziri Mkuu alilotoa kupitia Bunge lako tukufu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; pamoja na changamoto ya migogoro iliyopo kwenye hii mipaka, lakini bado tembo wamekuwa wanavuka kutoka kwenye eneo lao la pori tengefu kwenda kwenye makazi ya wananchi na kula mazao na kuvamia makazi na hivi sasa hawana chakula tena.

Ni lini mtawalipa wananchi hawa kwa kuangalia hali halisi ya sasa badala ya kufuata sheria ya wanyamapori ambayo inawaumiza wananchi wetu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Aida Khenani, Mbunge wa Nkansi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Pori la Akiba la Rwafi ni pori ambalo kabla ya kuanzishwa lilikuwa chini ya Halmashauri. Baada ya Halmashauri kushindwa kulisimamia vizuri lililetwa katika Wizara ya Maliasili na Utalii na wakati huo huo wananchi walikuwepo ambao walikuwa hawaijui mipaka vizuri na wakahitaji kufafanuliwa mipaka.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa ninavyoongea zaidi ya kilometa 50 tayari zimeshaanza kuoneshwa kwa maana ya kuwekwa vigingi kwa kushirikisha wananchi. Kwa hiyo, nimuombe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kuwa zoezi hili linaendelea, wataalamu wataendelea kushirikisha

wananchi kuonesha mipaka halisi ya pori hilo ili waweze kutambua maeneo ambayo yamehifadhiwa.

Mheshimiwa Spika, na swali hili la pili kuhusiana na tembo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Nkansi kwamba kwa kuwa Serikali imeendelea kulipa kifuta machozi na kifuta jasho, nimtaarifu tu Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Nkansi tutaenda kulipa kifuta machozi kabla ya kuisha mwaka huu wa fedha, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Oran Njeza, swali la nyongeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa fursa ya swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, na mimi nilitaka kujua ni lini Serikali itatatua mgogoro kati ya Hifadhi ya Kitulo na wananchi wa Kijiji cha Kikondo, Kata ya Ilungu ambao ni
wa muda mrefu na viongozi wetu wa kitaifa walishatoa ahadi ya kutatua huo mgogoro na kisha wananchi walipwe fidia? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Oran Njeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Hifadhi ya Kitulo ina changamoto, kuna migogoro kati ya hifadhi na maeneo ya wananchi, lakini zoezi hili liliingizwa kwenye Kamati ya Mawaziri Nane na hivi ninavyoongea baada ya Bunge hili kuisha, zoezi hili litaendelea kwenda kutoa ufafanuzi katika maeneo yaliyobaki ikiwemo Mkoa wa Iringa na Njombe ambapo kamati hii haijafika. Hivyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba zoezi hili tunaenda

kulitekeleza, tutaenda kutatua migogoro hii na wananchi waweze kuishi kwa amani.

**SPIKA:** Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, swali la nyongeza.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Image na Kata ya Ibumu, Kijiji cha Ilambo na Iyai kuna changamoto kubwa ya mipaka na kusababisha wananchi mara nyingi kugongana kwenye malisho.

Je, Wizara ina mpango gani wa kufika katika maeneo hayo na kutatua mgogoro huo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Justin Lazaro, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimuahidi tu Mheshimiwa Mbunge na wananchi wake kwamba nitaenda mimi mwenyewe kufanya ziara na kuzungumza na wananchi na kutatua changamoto hii.

**SPIKA:** Mheshimiwa Daniel Awack, swali la nyongeza.

**MHE. DANIEL A. TLEMAI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, Kata ya Endamaghang na Kijiji cha Endamaghang kuna mgogoro uliodumu muda mrefu na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro toka mwaka wa 2003. Sasa ni lini Serikali itaweza kutatua mgogoro huo ambao umedumu tangu mwaka 2003 mpaka leo hii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Daniel Awack, Mbunge wa Karatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tuna migogoro mipya na migogoro ambayo Kamati ya Mawaziri Nane inaendelea kuitatua. Kwa hii migogoro mipya nimuahidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tumeendelea kuhamasisha maeneo yote ambayo yana migogoro hii tuanze pia kuyapitia upya na kuyatolea ufafanuzi ikiwemo kutatua au kutafsiri mipaka kati ya ramani za vijiji na ramani za hifadhi.

Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge tutafika katika eneo lake ili tuweze kutoa ufafanuzi na pale ambapo itaonekana ramani zimeingiliana, basi Wizara ya Ardhi watatatua changamoto hii na tutaendelea kuhifadhi maeneo yaliyohifadhiwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, swali la nyongeza.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru na nakiri kwamba Mheshimiwa Waziri alishakuja jimboni kwangu akaona matatizo ya Kata yangu ya Mahoro, Kalemawe na Ndungu, lakini zaidi ya wananchi 300 ambao mazao yao yamevurugwa sana kwenye mashamba na hawana chakula sasa hivi hawajalipwa chochote tangu mwaka 2021. Na wananchi wangu wawili wameuawa na tembo, hawajalipwa chochote tangu mwaka 2021, Mheshimiwa Waziri nitakuletea *list* yote leo; je, unaniahidi utawalipa lini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Anne Kilango, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge, hivi ninavyoongea sasahivi hapa nikitoka hapa tu naenda kufuatilia, ili wananchi wa Same waweze kulipwa madai yao ya kifuta machozi na kifuta jasho. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Phillipo Mulugo, swali la nyongeza.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kuniona, naomba niiulize Serikali kwa kuwa Tume ya Mawaziri Nane haijawahi kufika Songwe na nimekuwa nikielezea hili jambo kila wakati.

Je, Tume hiyo baada ya kumaliza Bunge, iko radhi kufika Songwe katika Vijiji vya Gua, Nangwala, Kapalala, Udinde, Mkwajuni, Patamela, Saza na Mbangala kwa ajili ya kulinda mipaka ile ya maliasili, hasa *TANAPA, TAWA* na *TFS* katika maeneo ya wachimbaji wadogo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mulugo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mzungumzaji hajasema kama hivyo vijiji vina migogoro, nimhakikishie tu kwamba vile ambavyo viko ndani ya Kamati ya Mawaziri Nane, Kamati ya Mawaziri Nane watafika bila kuchelewa, lakini kama ni migogoro mipya tunaiomba ili tuweze kuiingiza kwenye

orodha ya migogoro mipya ili tuandae tena utaratibu wa kwenda kushughulikia migogoro hiyo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deus Sangu, swali la nyongeza.

Ngoja Mheshimiwa Deus Sangu, Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa fursa, kwanza nishukuru kwa majibu mazuri aliyoyatoa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, napenda tu niwafahamishe Waheshimiwa Wabunge kwamba ile Kamati ya Kisekta ya Mawaziri Nane, Wizara ya Ardhi ndio Mwenyekiti wa Kamati hiyo. La msingi tunalofanya si kwamba tutafika kila Kijiji, ni kwamba majukumu haya pia tunawapa mikoa ambayo ndio wanajua maeneo yao vizuri. Na sisi tunapokwenda tunazungumza na mikoa, wanatoa programu yao, pale ambapo wanakuwa wanahitaji uongozi wa ngazi za Wizara ndipo tunakwenda, lakini majukumu yote yanabebwa na mikoa husika kama mamlaka za utawala katika maeneo yale.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Deus Sangu, swali la nyongeza.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa fursa ya swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, nataka muuliza Mheshimiwa Naibu Waziri; je, ni lini mtamaliza mgogoro uliopo kati ya Kata ya Nankanga, Kipeta na Kilangawani kwa Pori la Akiba lile la Uwanda na wewe mwenyewe ulikuja ukajionea mgogoro ule ambavyo unawatesa wananchi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Malisili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Deus Sangu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli nilifika katika eneo hili ambapo kulikuwa kuna changamoto kati ya hifadhi kwa maana ya maeneo ya Ziwa Rukwa pamoja na wananchi wanaoishi maeneo hayo. Lakini nimuombe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba ufafanuzi tuliutoa na tutaendelea kuutoa, na tutafika pale kuendelea kutoa ufafanuzi kwa sababu maeneo yale tunayahifadhi kwa ajili ya kuzuia wavuvi kusogea kwenye maeneo ambayo ni mazalia ya samaki.

Mheshimiwa Spika, wananchi wengi wanataka wafike wavue kwenye maeneo ambayo mwisho wa siku watajikuta wanakosa mazao ya samaki. Hivyo, hata wananchi tunapaswa kuwaeleza ukweli kwamba kuna maeneo ambayo yanahifadhiwa kwa ajili ya faida yao wenyewe. Tutafika, tutatoa ufafanuzi, lakini wananchi wanatakiwa wafahamu tunatunza kwa ajili ya matumizi ya wao wenyewe wananchi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali langu ni kuhusu Nusu Maili; Nusu Maili ambayo ni eneo la Nusu Maili kuanzia vijiji kwenda kwenye hifadhi inayozunguka Mlima Kilimanjaro liliwekwa mwaka 1923 na Serikali za wakoloni.

Naomba nijue kwamba hii Kamati ya Mawaziri Nane imefikia muafaka gani kuhusu hilo eneo kwa sababu kuna

mkanganyiko mkubwa sana kuhusiana na maagizo ya Waziri aliyekuwepo Mheshimiwa Jumanne Maghembe na hali ilivyo sasa hivi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo ambayo tunatamani sana wananchi wafahamu kwamba ni maeneo ya muhimu. Eneo hili la Nusu Maili ni eneo ambalo tumeukinga Mlima Kilimanjaro ili barafu yake isiendelee kuyeyuka. Tumeendelea kuwaelimisha wananchi namna ambayo tunaweza tukafanya kama ni mbadala, badala ya kuendelea kuomba Nusu Maili, sisi tumejipanga kugawa miche kwa ajili ya wananchi wapande miti ili iweze kuwasaidia baadae kuwa na mavuno ya zao la miti ikiwemo kupata mkaa na matumizi ya nishati mbadala.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niendelee kuwaomba wananchi wanaozunguka Mlima Kilimanjaro. Mlima Kilimanjaro tunapata faida kubwa sana ikiwemo kupata watalii na hata wenyeji walioko katika maeneo hayo wanafaidika ikiwemo sisi kupeleka *CSR* kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, hii *Half Mile* ambayo tumeendelea kuiomba tuwaombe kwamba Mlima Kilimanjaro unahitaji kuhifadhiwa vizuri kwa ajili ya kizazi hiki na vizazi vinavyokuja. Kwa hiyo, niwaombe wananchi wanaozunguka Mlima Kilimanjaro tuendelee kushirikiana na Serikali kuutunza mlima huu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 468

**Kumaliza mgogoro wa Vijiji na Hifadhi ya Tarangire**

**MHE. DANIEL B. SILLO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itamaliza migogoro ya mipaka kati ya Vijiji vya Vilima Vitatu, Mwada na Ngolee dhidi ya Hifadhi ya Tarangire?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Sillo Baran, Mbunge wa Babati Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uwepo wa changamoto za migogoro katika Hifadhi ya Taifa Tarangire na baadhi ya vijiji vinavyozunguka hifadhi hiyo. Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi tutatuma wataalam kwenda kufafanua au kutafsiri mipaka ili wananchi wajue maeneo ya vijiji na kuheshimu mipaka ya hifadhi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, swali la nyongeza.

**MHE. DANIEL B. SILLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; kwa kuwa migogoro hii husababishwa na wahifadhi kutokushirikisha viongozi au wananchi wa maeneo husika wakati wanapoongeza mipaka hii ya hifadhi.

Je, Serikali haioni ni muhimu sana kuwashirikisha viongozi na wananchi wa maeneo husika, ili kupunguza igogoro hii ambayo imedumu kwa muda mrefu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kufanya ziara katika jimbo langu, hasa maeneo haya yenye migogoro ya mipaka na vijiji vyetu na kufanya mkutano mikutano ya hadhara, ili wananchi waeleze na ikiwa ni sehemu ya utatuzi wa migogoro hii? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyomgeza ya Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kumekuwa na changamoto hii ya namna ya kutafsiri mipaka na imesababisha wananchi kutoidhishwa na utatuzi huu. Nimuahidi Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Babati Vijijini kwamba tutafika na kuwashirikisha wananchi kutatua na kutafsiri mipaka ya eneo hili.

Mheshimiwa Spika, swali lingine ni utayari wa Wizara, akiwemo Waziri; tuko tayari kwenda kutoa ufafanuzi, lakini pia na kuzungumza na wananchi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali langu ni kwamba, je, ni lini Serikali itamaliza migogoro kati ya wanavijiji wa vijiji vya Nakingombe, Mtepela pamoja na Zinga Kibaoni dhidi ya Pori la Akiba la Selous katika Wilaya ya Kilwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Francis Ndulane, Mbunge wa Kilwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli mgogoro huu tunautambua na niliwahi kufanya ziara katika maeneo hayo. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tutafika kutatua mgogoro huu ikiwemo kutoa ufafanuzi kwa wananchi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana. *(Makofi)*

Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Juma Usonge Hamad, Mbunge wa Chaani, sasa aulize swali lake.

Na. 469

**Kupunguza kodi bidhaa za chakula zinazopelekwa Zanzibar**

**MHE. JUMA USONGE HAMAD** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kupunguza kodi, tozo na ushuru wa bidhaa za chakula/mboga kutoka Tanzania Bara kwenda Zanzibar?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Hamad Chande, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Usonge Hamad, Mbunge wa Chaani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, bidhaa za chakula na mbogamboga halisi zinazotoka Tanzania Bara kwenda Zanzibar hazitozwi kodi, tozo na ushuru wa aina yoyote kwa mujibu wa sheria, lakini bidhaa za chakula kutoka viwandani hutozwa tozo ya uchakataji nyaraka za forodha ya asilimia 0.6 tu kwenye thamani ya mzigo huo. Lengo la tozo hii ni kugharamia huduma ya uchakataji wa nyaraka za forodha na hutozwa kwa wateja wote wanaotumia mfumo wa forodha.

Mheshimiwa Spika, bidhaa za chakula na mbogamboga halisi hazitozwi tozo ya uchakataji wa nyaraka kwa sababu, hazihitaji kufanyiwa mchakato wa nyaraka katika mfumo wa forodha, ahsante.

**SPIKA:** Haya, nadhani majibu yameeleweka, Mheshimiwa amekaa.

Waheshimiwa Wabunge, ukiwa na swali la nyongeza unasimama hata kama swali lako ni la msingi, lazima usimame kuonesha unalo swali la nyongeza. Mheshimiwa Juma Usonge, swali la nyongeza.

**MHE. JUMA USONGE HAMAD:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa bidhaa ambazo tayari za mifugo hususan ng'ombe pamoja na mbuzi kwa Zanzibar ni adimu sana, lakini pia bei yake inakuwa ni ghali sana. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuhakikisha kwamba kufuta, lakini pia kupunguza kodi zote zile ambazo zinakuwa-

*charged* pale bandarini kwa upande wa Tanga pamoja na Kitumbwi, bandari ya Tanga ili sasa kumpunguzia Mtanzania wa Zanzibar gharama nafuu bidhaa ile ya ng'ombe kama wa Bara?

Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili; je, ni lini hasa Mheshimiwa Waziri utapanga safari ya kwenda bandarini kwenda kushuhudia namna Watanzania wanavyolazimishwa kulipa kodi maeneo ya bandarini? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Juma Usonge Hamad, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la usafirishaji wa nyama ya mbuzi, ng'ombe na wanyama wengine ni kweli kwamba kupeleka Zanzibar ni nyama adimu, haipatikani sana, lazima tuwe tunavusha kutoka Bara kwenda kule, lakini suala la ufutaji wa kodi na tozo naomba hili tulichukue tulifanyie mchakato kwa sababu ni suala la kisheria.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, kwenda kutembelea kuona hali halisi; naomba niambatane mimi na yeye mara tu Bunge hili litakapomalizika twende tukatembelee katika sehemu husika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya..., aah, bado swali moja; Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mbunge wa Kisesa, sasa aulizwe swali lake.

Swali la pili, je, ni lini hasa Mheshimiwa Waziri utapanga safari ya kwenda bandarini kushuhudia namna Watanzania wanavyolazimishwa kulipa kodi maeneo ya bandarini? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Juma Usonge Hamad kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la usafirishaji wa nyama za mbuzi, ng'ombe na wanyama wengine ni kweli kwamba kupeleka Zanzibar ni nyama adimu hazipatikani sana, lazima tunavusha kutoka bara kwenda kule. Lakini suala la ufuataji wa kodi na tozo naomba hili tulichukue tulifanyie mchakato kwa sababu ni suala la kisheria.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kuhusu kwenda kutembelea ili kuona hali halisi naomba niambatane mimi na yeye mara tu Bunge hili litakapomalizika tuende tukatembelee katika sehemu husika. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, bado swali moja Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mbunge wa Kisesa sasa aulize swali lake.

Na. 470

**Ukaguzi wa miamala ya uhamishaji bei ya mauziano (*transfer pricing*)**

**MHE. LUHAGA J. MPINA** aliuliza:-

Je, ni kwa kiwango gani Serikali imejiimarisha kukagua miamala ya uhamishaji wa bei ya mauzo ya bidhaa na huduma baina ya makampuni ya Kimataifa.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mbunge wa Kisesa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TRA* imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kiukaguzi wa miamala ya uhamishaji wa bei ya mauzo ya bidhaa na huduma baina ya makampuni ya Kimataifa kwa lengo la kuzuia upotevu wa mapato. Hatua hizo ni pamoja na:-

(i) Kuendelea kuboresha mifumo ya ndani ya ukusanyaji kodi kama vile Mfumo wa Usimamizi wa Mashine za Utoaji wa Risiti za Kielektroniki na Mfumo wa Kuwasilisha *return* Kielektroniki;

(ii) Kutoa mafunzo ya vitendo kwa watumishi katika nchi mbalimbali zenye uzoefu wa kushughulikia miamala ya uhamishaji wa bei ya mauzo ya bidhaa na huduma baina ya makampuni ya Kimataifa;

(iii) Kuimarisha utekelezaji wa mkataba wa kubadilishana taarifa kati ya Serikali ya Tanzania na nchi nyingine;

(iv) Kuendelea kufanya majadiliano na wadau mbalimbali ili kuona uwezekano wa kujiunga na *Global Forum on Tax Transparency* na ubadilishanaji wa taarifa kwa lengo la kupanua wigo wa upatikanaji wa taarifa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina swali la nyongeza.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri kwa kweli ya Naibu Waziri lakini ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, maboresho aliyoyasema Mheshimiwa Naibu Waziri ni makubwa. Je, hayo maboresho yametusaidia kuongeza kaguzi kiasi gani ikilinganishwa na kaguzi zilizokuwepo ambayo ilikuwa ni asilimia 1.2 kati ya makampuni 504 yanayojihusisha na miamala ya *transfer pricing?*

Swali la pili, Je, maboresho hayo yaliyofanywa na *TRA* yametuwezesha kuokoa fedha kiasi gani zilizokuwa zinapotea kutokana na kukosekana uwezo ndani ya nchi wa kukagua miamala *ya transfer pricing*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, kama ifuatavyo:-

Maboresho hayo ambayo tumefanya kupitia *TRA* yameongeza asilimia 4.5, mwaka uliopita kabla kufanya maboresho hayo ilikuwa tuko asilimia 1.2 lakini sasa tuko asilimia 4.5 kwa hiyo ni hatua kubwa sana ambayo tumepiga.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili ni suala la kitakwimu naomba tumpelekee kwa maandishi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia Issay swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali katika huduma za miamala hapa kwetu nchini, mara nyingi mashine za huduma kwenye maeneo ya huduma za fedha, zinaonyesha kwa muda huu hatutakuwa na huduma ya upatikanaji wa risiti.

Je, kama ni tatizo la kimfumo Serikali haioni kuwa inapoteza mapato?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama kulikuwa na tatizo hilo la risiti ilikuwa ni tatizo la muda mfupi na tayari tatizo hilo tumeshaliweka sawa. Sasa manunuzi yoyote yatakuwa yanatolewa risiti kwa njia ya elektroniki bila shaka nikutoe shaka Mheshimiwa Mbunge, kwa sasa hakutokuwa na mwanya wowote wa kupoteza mapato yetu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa George Mwenisongole.

Na. 471

**Ujenzi wa Kituo cha Polisi – Mji Mdogo Mlowo**

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE K.n.y MHE. JULIANA D. SHONZA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa kituo cha Polisi Mji Mdogo wa Mlowo baada ya kilichopo kuwekewa alama ya kubomolewa?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juliana Shonza, Mbunge wa Viti maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali itaanza ujenzi wa kituo cha Polisi Mji Mdogo wa Mlowo baada ya Halmashauri kuzingatia na kutekeleza maagizo ya Kamati ya Usalama ya Mkoa ambayo ni kupata eneo la kutosha, kujenga kituo na nyumba za Askari, Wakaguzi na Maofisa na kuandaa Hati Miliki ya eneo litakalopatikana.

**SPIKA:** Mheshimiwa George Mwenisongole swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri lakini naomba *commitment* ya Mheshimiwa Waziri.

Je, uko tayari kuongozana na sisi kwenda Mbozi kuangalia hali ya vituo vya Polisi na kuhusu ujenzi wa hicho kituo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwenisongole kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimepokea ombi lake na ninamuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya kujibu

swali hili tutakaa tupange ratiba mimi na yeye ya kuweza kutembelea kwenye Jimbo lake ili kuweza kukagua maendeleo ya vyombo vyetu vya usalama vilivyopo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani kwa ujumla wake.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deo Mwanyika swali la nyongeza.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Njombe hatuna Kituo cha Polisi ambacho kina hadhi ya Mkoa Polisi wanakaa kwenye nyumba mbalimbali ambazo zimetawanyika.

Je, ni lini sasa Serikali ina mpango wa kujenga kituyo kipya chenye hadhi ya Kimkoa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Deodatus Mwanyika Mbunge wa Njombe Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninamhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote ambao katika maeneo yao hakuna vituo vya Polisi, kwamba Serikali tumeanza jitihada hizo za kuhakikisha kwamba tuna kamilisha ujenzi wa Vituo vya Polisi katika ngazi zote kuanzia ngazi ya Mikoa, Wilaya, Kata.

Mheshimiwa Spika, nilipokuwa nimewasilisha bajeti yangu ya Wizara yangu mwaka huu wa fedha niliainisha juu ya mpango huo kabambe wa Serikali wa miaka 10, ambao

utahusisha ujenzi wa nyumba za Askari pamoja na vituo vya Polisi zaidi ya 51,000 nchi nzima.

Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba viko vituo ambavyo tutaanza navyo mwaka huu wa fedha na vingine vitafuata baadaye ikiwemo katika Jimbo la Mheshimiwa Mbunge aliyeuliza swali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu swali la nyongeza.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza swali moja kwamba Mji Mdogo wa Ngaramtoni katika Jimbo la Arumeru Magharibi umekuwa Mji Mkubwa kidogo na hauna Kituo cha Polisi chenye hadhi, inatumia nyumba ya Mtumishi wa Shamba la Mbegu.

Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi katika Mji Mdogo wa Ngaramtoni?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kama alivyozungumza Mheshimiwa Mbunge kwamba Mji wa Ngaramtoni hakuna kituo cha Polisi, hivyo kwanza nipongeze jitihada zilizochukuliwa na hasa za Mwananchi aliyejitolea kutoa jengo kwa ajili ya matumizi ya kituo cha Polisi.

Ninamuomba Mheshimiwa Mbunge kwamba jambo hili nilichukue ili tuone jinsi gani tunaweza kufanya kutatua changamoto hii, ikiwezekana kuangalia jitihada mbalimbali kwa kushirikiana nae Mheshimiwa Mbunge ya kuanza ujenzi wa Kituo cha Polisi katika eneo hili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza.

Je, ni lini Wilaya ya Kilolo itajengewa ofisi ya Makao Makuu ya Polisi kwa sababu ni muda karibu miaka 20 haijajengewa Makao yalipo Makuu ya Wilaya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jibu la swali hili linafanana na jibu ambalo nilijibu katika swali la mwanzo juu ya mikakati na jitihada za Serikali za kutatua changamoto za vituo vya Polisi katika ngazi mbalimbali ikiwemo Wilaya ya Kilolo. Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Mbunge avute subira wakati jitihada hizo zikiwa zinaendelea.*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Asha Abdullah Juma swali la nyongeza.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Kwa kuwa, uhitaji wa ujenzi wa vituo vya Polisi umekuwa mkubwa nchini; je, Serikali haioni umuhimu wa kuimarisha kikosi cha ujenzi cha Jeshi la Polisi na kuiga mfano kama wa Jeshi la Kujenga Taifa na Magereza katika ujenzi wa majengo yao, ambao pia utaokoa fedha nyingi za Serikali? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Asha Abdallah Juma kama ifuatavyo:-

Swali zuri la Mheshimiwa Mbunge, ni kweli kuna umuhimu huo lakini umuhimu huo tumeshaanza kuuona na kuufanyia kazi, kwa maana ya kwamba kupitia Shirika letu la Uzalishaji Mali la Jeshi la Polisi tumeanza jitihada za kuweza kufanya mageuzi makubwa ya shirika hili ili kuhakikisha linatoa mchango wake mkubwa katika kuendeleza miradi mbalimbali ya Jeshi la Polisi ikiwemo ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie kwamba moja katika mikakati hiyo ni kuimarisha kikosi chetu cha ujenzi ambacho hata hivyo hakiko katika hali mbaya sana, kwa sababu ziko shughuli ambazo zinafanywa na kikosi cha ujenzi cha Jeshi la Polisi, lakini nakubaliana na yeye kwamba kuna haja ya kufanyakazi ya ziada zaidi kukiimarisha kiwe bora Zaidi. Hilo jambo tunaendelea nalo na wazo lake tutaendelea kulifanyia kazi.*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Massay swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi.

Jimbo la Mbulu Vijijini Kata ya Yaeda Chini ulikuja Mheshimiwa Waziri ukatuhamasisha tukajenga Kituo cha

Polisi, sasa nguvu za wananchi pamoja na mimi tumeshindwa kujenga nyumba za Polisi. Utatusaidiaje kwenye bajeti hii ili nyumba hizo zipate kujengwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli mimi na yeye wakati nikiwa Naibu Waziri wa Wizara hii miaka kadhaa iliyopita tulishirikiana kuanza ujenzi wa kituo hiki. Kwa hiyo nichukue fursa hii kumpongeza yeye na wananchi wa Jimbo hilo kwa kuweza kutumiza ile ndoto tuliyokuwa nayo wakati tunaanza ujenzi huo na sasa hivi kituo kimekamilika.

Kwa hiyo nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba nguvu hizo za wananchi na nguvu zake hatuwezi kuziacha hivi hivi. Tumechukua suala la ujenzi wa Nyumba za Askari katika eneo hilo kwa uzito unaostahili na mimi nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kama tuliweza mimi na yeye kuanza jitihada za ujenzi wa kituo hicho, hatutashindwa mimi na yeye tukishirikiana kujenga Nyumba za Askari.

**SPIKA:** Mheshimiwa Subira Mgalu swali la nyongeza.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Kwanza naishukuru Serikali kwa ukarabati wa ofisi ya kituo kidogo cha Polisi Jimbo la Chalinze.

Kwa kuwa, Wilaya yetu ya Bagamoyo ofisi ya Polisi majengo yake ni ya muda mrefu na yamechakaa na kwa

kuwa tunatarajia watalii wengi kutokana na *Royal Tour* ambapo Mheshimiwa Rais alifika Bagamoyo.

Je, Serikali inatuahidi vipi katika kukarabati ofisi ya Polisi Wilaya ya Bagamoyo? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Kwanza ninapokea pongezi kwa niaba ya Serikali juu ya kazi ambayo tayari imeshaanza kufanyika kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge. Vilevile nichukue nafasi hii kutoa maelekezo kuwa tathmini ya ukarabati huo ufanyike ili tuweze kuangalia utaratibu wa kupata fedha kwa ajili ya kukarabati kituo hicho.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Maji Mheshimiwa Dkt Jasson Samson Rweikiza Mbunge wa Bukoba Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 472

**Ujenzi wa Mradi wa Maji Kemondo Maruku-Bukoba**

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA** aliuliza:-

Je, ni lini ujenzi wa Mradi wa Maji Kemondo - Maruku katika Jimbo la Bukoba Vijijini utakamilika.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza Mbunge wa Jimbo la Bukoba Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali inaendelea na utekelezaji wa awamu ya kwanza inayohusisha ujenzi wa chanzo cha maji na ulazaji wa bomba kuu kilometa nne na tenki la ujazo wa lita 3,000,000. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 utekelezaji wa mradi utaendelea na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2023.

Mheshimiwa Spika, mradi huo utanufaisha Kata Tano za Bukoba Vijijini ambazo ni Kemondo, Bujogo, Katerero, Maruku na Kanyangereko.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt Jasson Rweikiza swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali ambayo ni mazuri na nashukuru pia kwamba mradi unaenda vizuri kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri. Sasa maswali mawili:-

Swali la kwanza ni nini kauli ya Serikali kuhusu bei ya maji maana hata kule ambako miradi imekamilika kuna mahali ambako bei ya maji ni kubwa sana hadi shilingi 5,000 kwa *unit* ambazo ni lita 1000, kama kule Kyamurairi na sehemu nyingine ambako maeneo mengine ni shilingi 1000 lakini kule ni shilingi 5,000.

Swali la pili, kuna Kata Sita ambazo nako kuna mradi unaosemwa siku nyingi Kata ya Izimbya, Kaitoke, Mugajwale, Ruhunga, Katoro na Kaibanja, ambako Mheshimiwa Naibu Waziri amewahi kufika tukazungumzia jambo hilo na

anazifahamu Kata hizo, mradi huo unaanza lini kutekelezwa? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jasson Rweikiza kama ifuatavyo:-

Awali ya yote ni kweli nilifika na Mheshimiwa Mbunge nakupongeza, tulifanya hii kazi kwa pamoja na tutakuja tena kuona kwamba tunakamilisha miradi hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na bei za maji ninaomba kutoa taarifa ni wiki ya jana tu Mheshimiwa Waziri ametoa bei elekezi kwa miradi yote nchi nzima. Hivyo maeneo ambayo yana bei ambazo kidogo siyo rafiki kwa wananchi kama maeneo yako ya Bukoba Vijijini, hata pale Karatu yote tumeyazingatia na bei elekezi zimetolewa na Mheshimiwa Waziri kwa kuzingatia nguvu inayotumika kusukuma mitambo yetu. Kama ni mafuta, kama ni umeme wa jua kama ni mserereko, kama ni umeme wa *TANESCO* pamoja na *pump* za mikono, yote haya Mheshimiwa Waziri ameshatoa maelekezo na sasa hivi bei zitakwenda kuwa rafiki sana, wiki ijayo kwa maana ya mwaka mpya wa fedha zitaanza kutumika.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kuhusiana na Kata Sita alizozitaja Mheshimiwa Mbunge tumeshirikiana kwa pamoja na tayari usanifu nafahamu unaendelea, kadri tutakavyopata fedha tutaleta Mkandarasi mapema sana ili Kata hizi zote ziweze kupata maji na maeneo haya ambayo kwa muda mrefu yamekuwa yakipata matatizo ya maji tunakuja kuyashughulikia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dorothy Kilave swali la nyongeza.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mkoa wa Dar es Salaam miundombinu yake ya maji ni ya muda mrefu sana, kwa sababu tulipata maji muda mrefu kabla ya Mikoa yote. Sasa hivi miundombinu ile ni mibovu na inamwaga maji mengi hasa katika Jimbo letu la Temeke.

Je, Serikali mna mkakati gani wa kuelekeza tena upya miundombinu ya maji katika Mkoa wetu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dorothy Mbunge wa Temeke, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna baadhi ya maeneo ya Temeke yana changamoto ya mabomba kupasuka kwa uchakavu na maji sasa yamekuwa mengi kwa sababu ni miradi mikubwa iliyotekelezwa na *DAWASA*, hivyo nipende kukutoa hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari tumeanza utekelezaji nimeshafuatilia hili maeneo ya Tandika, Tandale maeneo ya Wailess na Temeke penyewe tayari wameanza kubadilisha yale mabomba yaliyochakaa.

Mheshimiwa Spika, maeneo ambayo bado maji yanaendelea kuvuja tunaendelea kufanyia kazi na kadri tutakavyopata fedha tunakuja kukamilisha maeneo yote ambayo maji yanavuja. Hili siyo tu kwa Temeke Waheshimiwa Wabunge niseme Mikoa yote, Majimbo yote tumetoa maelekezo kuhakikisha maeneo ambayo maji sasa yamekuwa ni mengi na mabomba yamechakaa yanashindwa kuhimili presha ya maji haya, tunakuja kufanyia ukarabati.*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Shamsia Mtamba, swali la nyongeza.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Tatizo lililopo Bukoba Vijijini linafanana kabisa na tatizo lililopo Mtwara Vijijini. Kata ya Mango Pacha Nne, kuna mradi wa maji hadi leo haujakamilika. Je, ni lini Serikali itamalizia mradi huu ili kumtua ndoo kichwani mama wa Mango Pacha Nne ambaye kwa muda mrefu wamekuwa na changamoto kubwa ya maji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shamsia, Mbunge wa Mtwara Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge amefuatilia hili sana na nimhakikishie nitafika Mtwara vijijini lakini tayari naendelea kusisitiza maelekezo tuliyoyatoa kwa watendaji wetu waweze kufanya kazi usiku na mchana ili mradi ule uweze kukamilika na akinamama na familia zote za Mtwara Vijijini ziweze kunufaika na kazi nzuri inayofanywa na Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan. Tunampongeza Mama Samia tumeshapata fedha asilimia 95 ya bajeti ambayo tunakwenda kuimaliza hivi punde. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kasalali Mageni, swali la nyongeza.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru mradi wa maji wa Isunga Kadashi ni moja ya miradi ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri aliitembelea katika Jimbo la Sumve na tukaahidiwa kwamba mradi ule utaanza kutoa maji ndani ya miezi miwili, lakini hadi sasa ninapozungumza ni zaidi ya mwaka sasa umepita na mradi ule hautoi maji.

Je nini tamko la Serikali kuhusu kitendo hicho ambacho kinapelekea watu wa Kijiji cha Isunga kutokupata maji kwa muda? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Sumve, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tamko la Serikali kwenye mradi ambao mimi na Mheshimiwa Mbunge tuliutembelea ni kufuatilia na kuhakikisha maji yanatoka, Mheshimiwa Mbunge naomba niwe nimelipokea nilifanyie kazi kwa nini maji hayajatoka hadi sasa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhandisi Samweli Hhayuma swali la nyongeza.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kijiji cha Mrelu ni eneo kame sana na kimeshachimbwa kisima. Je, ni lini Wizara italeta fedha ili maji yale yaweze kusambazwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba arudie swali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hhayuma hujasikika vizuri.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kijiji cha Mrelu ni eneo kame sana na sasa hivi kisima kimeshachimbwa na wananchi wanaishukuru sana Serikali. Je, ni lini fedha zitapelekwa ili maji yale yaweze kusambazwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hhayuma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mara tunapopata chanzo cha uhakika, kusambaza ni moja ya wajibu wetu mkubwa na hiyo ndio tija ya dhima ya Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Mbunge mwaka ujao wa fedha mapema kabisa miezi ya mwanzoni tunaenda kusambaza maji katika eneo hili ambalo tumechimba kisima.

**SPIKA:** Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, swali la nyongeza.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mradi wa Nduku – Ntobo - Busangi ni mradi uliopangwa kiasi cha shilingi 750,000,000 ili uweze kukamilika na tayari hatua za manunuzi, mabomba yote ya plastiki yamenunuliwa, lakini kimekwamisha tu bomba za chuma.

Sasa je, ni lini Serikali itaenda kulipa fedha ili mabomba haya yaweze kununuliwa na mradi uweze kukamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama yeye alivyokiri ni mradi ambao unakwenda kuleta tija katika eneo hili na tayari baadhi ya mabomba yamefika, bomba hizi za chuma tayari zimeshaagizwa. Tumshukuru Mheshimiwa Rais ametoa fedha nyingi, kazi zimekuwa nyingi, hivyo hata wanaozalisha haya mabomba wamezidiwa, kwa hiyo kidogo kumekuwa na ucheleweshwaji. Hata hivyo, tumeshawaongezea nguvu ya

kuona kwamba wanaweza kufanikiwa kuleta mabomba haya ndani ya muda. Hivyo, tunaomba Mheshimiwa Mbunge avute Subira, mabomba ya chuma yanakuna na kazi hii lazima ikamilike.

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, Mbunge wa Ushetu, sasa aulize swali lake.

Na. 473

**Kupeleka maji ya Ziwa Victoria- Ushetu**

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka maji ya Ziwa Victoria katika Halmashauri ya Ushetu?

.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, Mbunge wa Ushetu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali imekamilisha ujenzi wa Miradi ya Maji katika Vijiji vya Kisuke, Igunda na Nyankende. Vilevile utekelezaji wa Miradi ya Maji katika Vijiji vya Mpunze, Sabasabini, Iponyanholo, Itumbili, Mitonga na Ididi inaendelea na inatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2022. Kukamilika kwa miradi hii kutaboresha huduma ya upatikanaji wa maji toka asilimia 58 hadi asilimia 62. Aidha, mpango wa muda mrefu ni kutekeleza mradi utakaotumia chanzo cha maji cha Ziwa Victoria ambapo usanifu utafanyika katika mwaka wa fedha 2022/2023.

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa maji pamoja na timu yake yote kwa kazi nzuri wanayoifanywa kwa miradi ya maji, lakini nina maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, Mkoa wa Shinyanga una Majimbo sita na Jimbo la Ushetu ni mojawapo lakini Majimbo matano yana miradi mikubwa ya maji ya Ziwa Victoria isipokuwa Jimbo la Ushetu ambalo ni kilometa kama 17 tu ilipo miradi mikubwa wa maji. Leo hii maji hayo yameenda Tabora, yameenda Shelui, Mkoani Singida. Sasa nataka nipate *commitment* ya Serikali ni lini sasa maji haya ya Ziwa Victoria yataanza kupelekwa kwa wananchi wa Jimbo la Ushetu?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari kuongozana na mimi kwenda kushuhudia adha wanayoipata wananchi wa Jimbo la Ushetu hasa katika Kata za Uyogo, Mapamba, Ushetu, Ulowa, Ubagwe na Ulewe ambako sasa wanauziwa ndoo ya maji kwa shilingi 1,500 hadi 2,000? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Emmanuel Cherehani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napokea shukrani za Mheshimiwa Cherehani. Naamini anafahamu wiki iliyopita tayari watendaji wetu kutoka Makao Makuu ya *RUWASA* walikuwa jimboni kwake na chanzo cha wale watendaji kufika pale ni kwa sababu tunaenda kuanza mradi huu

ambao tutachukua maji ya Ziwa Victoria kuleta kwenye maeneo haya ambako miradi inahitajika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kuongozana na Mheshimiwa Mbunge nilishamjibu kwamba baada ya watendaji wetu wataalam wakishamaliza eneo lao, nitakwenda kuongeza hamasa ya kuona miradi hii inatekelezwa ndani ya muda uliopangwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Venant Daud Protas, swali la nyongeza.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Tarehe 29 mwaka 2021 niliuliza swali la msingi juu ya mradi ya Ziwa Victoria wa kwenda Kata za Goweko, Igalula na Nsololo na majibu ya Serikali hadi kufikia Juni, 2022, utakuwa umekamilika, lakini mradi huu upo asilimia 30. Nataka kauli ya Serikali, je, mradi huu utakamilika lini na wananchi wa Kata za Kigwa, Goweko na Nsololo wataweza kupata maji ya Ziwa Victoria?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Venant Protas, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Mheshimiwa Mbunge amekuwa akifuatilia sana huu mradi, lakini changamoto za kiufundi ndizo zilizopelekea mradi huu kusuasua na sasa hivi ufumbuzi umeshapatikana. Mheshimiwa Mbunge kama tulivyoongea avute subira tunakwenda kukamilisha mradi huu na lengo ni kuona wananchi wanapata maji safi, salama na ya kutosha tena bombani.

**SPIKA:** Mheshimiwa Miraji Mtaturu, swali la nyongeza.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, ahante sana kwa kunipa nafasi. Chanzo cha maji cha Lojo kilichopo katika Kijiji cha Matongo pale Ikungi ni chanzo kikubwa ambacho kilifanyiwa utafiti mwaka 2010.

Je, ni lini sasa Serikali itaweza kukiendeleza chanzo kile ili kiweze kutosheleza maji katika Mkoa mzima wa Singida? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Miraji Mtaturu, Mbunge wa Ikungi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli chanzo hiki tunakitarajia kuwa ni moja ya vyanzo vitakavyopunguza tatizo maji katika eneo lake. Kukiendeleza chanzo hiki mwaka ujao wa fedha tutarudi kuona namna bora ya kutumia maji haya. Lengo ni kuona kwamba tunapunguza tatizo la maji katika eneo lake lote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Wilaya ya Muleba na hili swali nimeuliza mara nyingi sana hapa Bungeni. Tunapakana na Ziwa Victoria na Wilaya ya Muleba ina matatizo makubwa sana ya maji pamoja na kwamba tupo kando kando ya Ziwa Victoria. Tuna mradi ambao usanifu na upembuzi yakinifu umekamilika wa kuchota maji kutoka ziwa Victoria na kuyasambaza kwenye Kata sita za Gwanseli, Magata, Kabuganga, Muleba Mjini, Buleza, Kagoma na Kikuku. Je, ni lini utekelezaji wa huo mradi utaanza kwa ajili ya wananchi wa Wilaya ya Muleba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ishengoma Kikoyo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru kwa kukiri kwamba pamoja na changamoto hizo lakini kazi zinaendelea kufanyika ndani ya Jimbo lake na hizo kata zote alizozitaja tunaendelea kuzifanyia kazi. Mimi na Mheshimiwa Mbunge tulitembelea chanzo kile kingine pale Kizuri ambacho kinatoa maji mengi na tunakiboresha. Kutumia maji ya Ziwa Victoria tutayatupia kwenye maeneo haya yote ambayo yapo mbali na vyanzo vingine. Maeneo yale ambayo Mheshimiwa Mbunge tumeshaongea mara nyingi na nimefika pale, ambayo yanapata maji tutaendelea kutumia vyanzo vilivyopo. Kwa maeneo ambayo ni muhimu kutumia maji ya Ziwa Victoria, tunakwenda kufanya kazi nzuri na maeneo haya yote aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge tutahakikisha maji yanapatikana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Pallangyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Mradi wa Maji wa Patandi unaotekelezwa katika Kata ya Keri umeacha vitongoji vinne katika Kata ya Gwarusambo ambako ndiko vyanzo vya maji vinapatikana.

Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kuambatana nami kwenda *site* kutatua hizo changamoto? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Pallangyo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimeshafika Jimboni kwa Mheshimiwa Dkt. Pallangyo na tumefanya kazi nzuri, maeneo ambayo hayakupata maji kwa miaka mingi sasa hivi yanapata. Hivi vitongoji vinne vilivyobaki navyo vinaenda kwenye mwaka ujao wa fedha na vitapata maji. Suala la mimi kufika Jimboni kwa Mbunge, asijali kama ambavyo nilikwenda nikimaliza maeneo ambayo sijafika, nitarudi tena.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na sasa nilete matangazo niliyonayo hapa mbele.

Kwanza ni wageni waliopo Jukwaa la Spika, na hawa ni wageni 20 wa Bunge ambao ni walimu wa Shule ya Sekondari Uyole kutoka Jijini Mbeya wakiongozwa na Mwalimu Sela Mwalyambi na kikundi hiki kinalea watoto wanaoishi katika mazingira magumu, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge ambao wamealikwa pia kuja Bungeni wageni wa Waheshimiwa Wabunge tusimame wote kwa pamoja, karibuni sana wageni wetu, tunaamini mmewaona Wabunge wenu wakiwawakilisha vizuri hapa ndani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wengine waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; kwanza ni wanafunzi 120 na walimu 10 kutoka *Peace Land English Medium School ya* Ukerewe, Mkoani Mwanza, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tunao wanafunzi 67 wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Huruma kutoka Jijini Dodoma wakiongozwa na Mkuu wa Shule hiyo Ndugu Chrispiana Ikaku, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo pia Mgeni wa Bunge na huyu ni Shekhe Alhaji Salim Mbarak Mtimkavu, Mwenyekiti wa Taasisi ya Kadiriya Taifa, kiongozi wetu anatokea Arusha, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo lingine hasa ili tangazo linatoka kwangu mimi mwenyewe.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kwamba tumekuwepo hapa Bungeni tangu mwezi Machi, 2022, ambapo katika kipindi hicho tumefanya kazi nyingi pamoja na kupokea mapendekezo ya Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Vilevile tumefanya ziara za Ukaguzi wa Utekelezaji wa Miradi ya Serikali katika maeneo mbalimbali nchini.

Pia tumekaa vikao vya Kamati na kuchambua Bajeti za Wizara Waheshimiwa Wabunge nawageukia mpo wengine mnaongea nikiwa nimesimama, lakini pia tumekaa vikao takribani vitakuwa 55 hadi siku ya Alhamisi tutakapohitimisha Mkutano huu wa Bajeti.

Waheshimiwa Wabunge, shughuli hizo tulizozifanya zimewezesha kupitisha kwa ufanisi kwa bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2022/2023, kwa kuzingatia hilo na kwa kuwa tumefanya kazi hii kwa muda mrefu, nimeona ni vema tuwe na siku ya kujumuika pamoja na kuhitimisha Mkutano wetu wa Bajeti. *(Makofi)*

Hivyo Waheshimiwa Wabunge, siku ya kesho Jumatano tarehe 29 Juni, 2022, kutakuwa na Jambo la Wabunge na watumishi wa Bunge kuanzia saa 12.00 jioni kwenye viwanja vya Bunge. Jambo hili halitakuwa jepesi, litakuwa jambo zito, kwa hiyo tutakuwa na wageni mbalimbali, lakini na sisi wenyewe si mnajua tukikusanyika huwa kuna vipaji mbalimbali, kwa hiyo vipaji mbalimbali vya humu Bungeni lakini pia kutokea kwa watumishi vitaoneshwa hiyo kesho.

Mgeni rasmi kwenye shughuli hii anatarajiwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge na watumishi wote kesho saa 12 jioni tutakusanyika pale sehemu ya maegesho ya magari kwa hivyo Waheshimiwa Wabunge kesho yale maegesho yaachwe wazi muda wa mchana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunalo tangazo lingine linatoka kwa Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba leo siku ya tarehe 28 Juni, 2022, kutakuwa na Semina ya Wabunge wanawake wote mara tu baada ya kuahirisha kikao cha Bunge saa 7.00 Mchana. Semina hiyo itakuwa Ukumbi wa Msekwa. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge wanawake wote mnaombwa kuhudhuria Semina hiyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo tutaendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2022
### *(The Finance Bill, 2022)*

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na majadiliano, ninayo majina hapa ya Wabunge ambao wameomba kuchangia. Tutaanza na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha atafuatiwa na Mheshimiwa Mhandishi

Mwanaisha Ng'anzi Ulenge na Mheshimiwa Emmanuel Godwin Kunambi ajiandae.

**MHE. SHAMSI VUAI NAHODHA:** Mheshimiwa Spika, nchi yetu imebarikiwa na Mwenyezi Mungu kuwa na vivutio vingi sana vya utalii lakini kwa bahati mbaya idadi ya watalii wanaotembelea nchi yetu na kiwango cha mapato tunachokikusanya katika sekta hiyo hakilingani hata kidogo na uzuri wa nchi yetu. Zipo nchi tunazopatakana nazo zinavivutio vichache sana vya utalii lakini idadi ya watalii wanaotembelea nchi hizo na kiwango cha mapato wanachokikusanya ni kikubwa kuliko sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano wa karibu tu. Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inapata watalii 500,000 kwa mwaka, wakati sisi Tanzania Bara tunapata idadi ya watalii 800,000. Zanzibar inavivutio viwili tu vya utalii; magofu ya kihistoria na fukwe, lakini kwa maoni yangu hata Tanzania Bara vivutio hivyo vipo, magofu ya kihistoria yapo, fukwe mwanana zipo; Lindi, Mtwara na Mkoa wa Pwani; mbuga za wanyama. Sasa nahisi kuna tatizo mahali fulani. Ama takwimu za idadi ya watalii wanaotembelea nchi yetu hazikusanywi kwa usahihi, ama huduma zetu za utalii hazijafikia kiwango cha kuridhisha, ama huduma zetu za utalii ni ghali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napendekeza mambo yafuatayo ili kukabiliana na hali hiyo. La kwanza, Serikali iwaagize mabalozi wetu watupatie taarifa za hatua za kukuza utalii zinazofanywa katika nchi wanazofanyia kazi ili tujifunze yale mazuri wenzetu wanayofanya. Ushauri wa pili, Serikali iweke mifumo imara ya TEHAMA itakayoweza kukusanya taarifa sahihi za watalii na mapato ya Sekta ya Utalii na mifumo hiyo iunganishwe moja kwa moja na Wizara ya Fedha ili Wizara ya Fedha waweze kuiangalia. La tatu, Serikali iimarishe Chuo chetu cha Utalii ili kiweze kutoa huduma bora na zinazofikia kiwango cha Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna nchi moja jirani yetu wana chuo maarufu sana kinachoitwa *Utalii College*. Chuo hiki kimekuwa kikitoa wanafunzi wenye uweledi wa hali ya juu sana katika huduma ya utalii. Kwa maoni yangu, nadhani siyo vibaya tukajifunza mambo mema kutoka kwa majirani zetu. Tukitembelee chuo hicho ili tuone mambo waliyofanya vizuri na sisi tuyafuate ili tuweze kuimarisha chuo hiki.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, atafuatiwa na Mheshimiwa Emmanuel Godwin Kunambi na Mheshimiwa Cecil David Mwambe, ajiandae.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi hii ya kuchangia. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu Mwenye Enzi na Utukufu kwa kunisimamisha mahali hapa, muda na wakati kama huu.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii pia kuipongeza sana Wizara pamoja na Watendaji wake, na Mawaziri kwa kazi kubwa waliyofanya ya kuleta Muswada huu wa Marekebisho ya Sheria 38. Kipekee kabisa niipongeze sana Kamati ya Bajeti kwa marekebisho mazuri na kazi kubwa waliyoifanya kuhakikisha kwamba sheria hizi zinakwenda ku-*reflect* bajeti yetu na Serikali kuweza kutekeleza majukumu yake ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikijenga madaraja nchini na madaraja haya makubwa yamekuwa yakijengwa na matokeo yake tunategemea madaraja haya yaweze kudumu kwa mujibu wa muda wa usanifu uliopangwa. Tuliona hapa kumekuwa na mjadala kuhusiana na Daraja la *Tanzanite* kwamba lilipiwe au lisilipiwe na hatimaye Serikali ilitoa tamko kwamba Daraja la *Tanzanite* litalipiwa. Sasa kwa

*existing good practice,* nilitegemea kwamba Muswada huu wa Sheria ya Fedha unge-*reflect* hili jambo la Daraja la *Tanzanite* kwamba litalipiwa.

Mheshimiwa Spika, pia katika Muswada, hizo sheria 38 zilizoletwa, hakuna mahali nimeona *The Road and Fuel Act* ya 2019 *Cap* 220 kufanyiwa marekebisho ili kuingiza hili la Daraja la *Tanzanite* kulipiwa. Kwa sababu kwa mujibu wa sheria ile, madaraja haya ambayo yanafanyiwa matengenezo kwa sheria hii, *Cap*. 220. Sasa Serikali kuwa kimya, kutokulizungumzia hili katika Miswada hii inayorekebishwa, maana yake ni nini? Kwamba hili la kukusanya tozo katika Daraja la *Tanzanite* tutaliwekaje? Maana yake nini?

Mheshimiwa Spika, sasa kwa upeo wangu, naamini Serikali labda imepitiwa kuingiza hili katika Muswada huu ambao tunaujadili leo. Kwa hiyo, naomba kuikumbusha Serikali kwamba ione haja sasa ya Sheria hii ya *The Road and Fuel Tolls Act, Cap,* 220 kuweza kuiboresha ili ku-*reflect* hili la kukusanya tozo katika Daraja la *Tanzanite*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia naipongeza sana Kamati kwa dhamira yake njema na Serikali kuhakikisha inalinda haki za wasanii nchini. Kwa kuletwa marekebisho haya ya saba (*ammended of the copyright and neighbouring right acts, cap.* 218). Naipongeza sana kwa dhamira njema ya kutaka kuhakikisha wasanii wanapata haki zao inavyostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile kuongeza tozo katika vifaa vya kuhamishia ambapo ndiyo wameona ni namna pekee ya kuwakaba wale ambao wanaiba kazi za wasanii wasiweze kuhamisha kazi za wasanii kwa kutumia vifaa hivi, mimi naamini siyo sahihi kwa sababu vifaa hivi ambavyo ni *USB* na *harddisk,* na vitu vya namna hiyo ambavyo vinatumika pia na wanafunzi kote nchini katika kuindea taaluma zao, ndivyo vifaa vinavyotumika kuhakikisha

wanahamisha nyaraka mbalimbali za kitaaluma ili wanafunzi waweze kujisomea. Hata watendaji mbalimbali Serikalini wanatumia vifaa hivi kuhifadhi na kuhamishia nyaraka mbalimbali katika utendaji kazi. Hata wakufunzi wanatumia vifaa hivi hivi katika kuhakikisha kwamba wanaweza kupeleka elimu kwa vijana hawa wanaosoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa Serikali kuongeza tozo katika vifaa hivi, leo wanataka kusaidia wasanii, lakini kundi kubwa hili la wanataaluma na wanafunzi wameliangaliaje? Vifaa hivi kwa wanafunzi ni vifaa muhimu sana. Naomba Serikali iangalie namna ya kuhakikisha kwamba inalinda haki za wasanii bila kuathiri kundi kubwa la wanataaluma na wanafunzi ambao wanatafuta elimu katika Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, tumeona duniani kwote kuna sheria ile ya *plagiarism,* ya kuhakikisha wanalinda haki za watu, lakini sheria hii licha ya kwamba ipo, haijawahi kusema kwamba tafiti fulani iliyofanywa isiwe *publicized* ili mwanafunzi asiibe. Kuna namna ambayo wanatumia kuhakikisha kwamba haki za watu walizozitendea kazi tafiti zao zinahifadhiwa, mtu haruhusiwi kuziiba, lakini bila kuathiri maana pana ya wanataaluma kuweza kufanya *literature review,* ndiyo sababu zinaendelea kutangazwa kazi za watu mbalimbali lakini bila kuwabana wanataaluma kuendelea kuindea taaluma yao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba sana Serikali iliangalie hili. Suala la *USB Cables, harddisk* ni vifaa muhimu katika taaluma nchini. Tusilisahau kundi hili kubwa na kuangalia kundi lingine, tutafute namna ya kuona tutaweza kulinda vipi wasanii bila kuathiri hili kundi kubwa.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kwa dhamira yake kubwa na njema ya kuhakikisha kwamba itatekeleza mipango yake kwa haraka kwa kuangalia namna ambavyo wataweza kuongeza mikopo ya ndani wakati

tunasubiria kukusanya fedha yetu, wao wanaweza kukopa na kuweza kuendelea kutekeleza majukumu mbalimbali ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niishauri Serikali, hii ni namna nzuri kabisa ya kupata fedha, lakini kwa uzoefu wa nchi zetu jirani, wenzetu wameingiza *infrastructure bond,* kwa maana kwamba, vilevile Benki Kuu ya Tanzania tunaweza kupitia mifuko yetu mbalimbali ambayo inatekeleza na imepewa majukumu ya kukusanya tozo mbalimbali kuweza kuweka *infrastructure bond* na ambazo zitasaidia kutekeleza majukumu fulani mbalimbali ya Serikali ili kuweza kutekeleza kwa haraka. Kwa mfano Ghana, kupitia Mfuko wa Bodi ya Barabara wana *infrastructure bond*. Vilevile Kenya wameshaingiza kwenye sheria *infrastructure bond. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ili Serikali iweze kutekeleza majukumu yake kwa haraka hasa kwenye miradi ambapo kumekuwa na riba nyingi za Wakandarasi kwa sababu ya ucheleweshaji wa malipo, tafadhali naishauri Serikali, ione haja pia ya ku-*accommodate* katika hili na kuhakikisha inatafuta fedha ya kuzungusha mapema kabisa katika utekelezaji wa majukumu kuona haja ya kuweka *infrastructure bond.* Ni muhimu sana kwa sababu barabara nyingi hazifanyiwi matengenezo sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika bajeti iliyopita ya 2021 nakisi ya fedha ambayo ilipaswa kufanya matengenezo ya barabara ni asilimia 51. Kwa hiyo, kuna haja kabisa ya kuona haja kwanini tuweze kutafuta *infrastructure bond*.

Mheshimiwa Spika, nimerudia kulitamka hili, gharama ya *network* ya barabara zetu nchini ni kubwa mno, tayari imeshafika Shilingi trilioni 21. Kama Taifa tuna kila haja ya kulea sana barabara zetu hizi ziendelee kudumu. Kwa hiyo, naishauri Serikali, hapo katika kuingiza fedha za kufanya kazi

kwa haraka, kuizungusha fedha, ione umuhimu wa kuingiza *infrastructure bond*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo naomba kulizungumzia, tumeona Mheshimiwa Rais wetu mpendwa kabisa mama yetu rahimu, mkarimu, mama mlezi wa Taifa letu, ameshaifungua Tanzania na amedhamiria kuifanya Tanzania *the prominent tourism destination in the world*. Mama amefanya kazi kubwa sana ya kuheshimika kupitia *Royal Tour*. Nimeona hapa pia Serikali imeweka juhudi kuhakikisha kwamba zile ndege ambazo watalii watakuwa wanazitumia zisitozwe kodi. Naipongeza sana Serikali kwa hatua hii ambayo imeichukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kusisitiza jambo, kwamba Serikali katika kuhakikisha kwamba inataka ile azma ya Mheshimiwa Rais inatimia, ni pamoja na kuhakikisha viwanja vya ndege vyetu vinakuwa na ubora unaostahili. Ili kuhakikisha hili, (*International Civil Aviation Organization – ICAO)* imeshaweka utaratibu kwamba Mamlaka za Viwanja vya Ndege viwe na vyanzo vya mapato. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema, ninayo majina hapa ya wachangiaji. Kwenye ngazi hii, tuko kwenye kutunga sheria. Sasa hii sheria tunayoitunga tunatazama maeneo ambayo Serikali imeleta, maeneo ambayo Serikali imeafikiana na Kamati ya Bajeti kubadilisha, maeneo

ambayo Serikali haijaafikiana na Kamati ya bajeti kubadilisha. *(Makofi)*

Kwa hiyo, unaposimama kuchangia ngazi hii, huwezi kuchangia jambo jipya. Kwa nini? Kwa sababu tuko kwenye kutunga sheria. Kwa hiyo, ngazi hii ya kutunga sheria, kama umeleta marekebisho, unaweza ukayazungumzia sasa ili wenzio baadaye wakuunge mkono. Ile kwamba una hoja fulani hivi unataka kuisema Serikali iichukue, siyo ngazi hii. Ngazi hii tunatunga sheria. Kwa hiyo, unaangalia sehemu kwenye sheria ambapo kuna jambo la kusema, hili Serikali pengine imechukua, unataka kupongeza, haya. Hili Serikali haijaelewana na Kamati ya Bajeti, ningependa kuwashawishi Wabunge bado twende hivi, haya. Ndiyo ngazi hii tulipo. Kwa hiyo, siyo kwa ajili ya kuanzisha hoja mpya ambazo zinaweza kuchukuliwa na Serikali.

Mheshimiwa Emmanuel Godwin Kunambi, atafuatiwa na Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, ajiandae.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nianze moja kwa moja kujielekeza kwenye mchango wangu na nitaanza na eneo la ukurasa 19, eneo ambalo linazungumza kuhusu Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura Na. 148. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza Wizara, lakini pia kwa namna ya pekee kabisa nampongeza Mheshimiwa Rais. Tunaona dhamira njema ya Mheshimiwa Rais kuvutia wawekezaji ndani ya nchi yetu. Ukisoma eneo la namba ya kirumi ya tatu, kwa maana ya *roman three* kwenye ukurasa ule wa 19, kuna eneo limezungumzwa kwa Habari ya kumpa Waziri mamlaka ya kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani wawekezaji mahiri maalumu baada ya kupata ridhaa ya Baraza la Mawaziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utaona moja kwa moja hapa, dhamira ya Serikali ni kuvutia wawekezaji ndani na nje ya nchi. Nitoe mfano mmoja tu, nchi kama Dubai, miaka 40 iliyopita Dubai haikuwa hivi ilivyo leo. Ukiitizama Dubai, asilimia 80 ya uwekezaji waliofanya uwekezaji wa Mataifa ya kigeni. Leo hii tunakwenda kutalii Dubai kuangalia majengo, lakini ukiangalia uwekezaji wa Dubai mwingi kwa asilimia 80 umefanywa na Mataifa ya kigeni. Kwa hiyo, naona hapa tunakwenda kuona Taifa letu linakwenda kubadilika kwa kasi sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo eneo hili naunga mkono. Ikikupendeza, nitarudi kidogo kwenye eneo hili. Jambo hili ni muhimu. Tuna miradi yetu hapa nchini; tuna miradi ya maji, tuna miradi ya umeme, tuna miradi ya barabara, lakini miradi hii kwenye mikataba kuna baadhi ya maeneo kuna takwa la kuomba kibali, kama kuna mkataba unasema, Kibali cha Msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa Wakandarasi.

Mheshimiwa Spika, kibali hiki kinaombwa na *client,* yaani taasisi inayoomba iliyompa Mkandarasi kazi, ndio anaomba kibali cha kusamehewa Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)*. Kwa bahati mbaya zaidi, eneo hili kibali hiki kinaombwa kwa mtu mmoja tu, Kamishna *General* wa *TRA*. Nilijaribu kujiuliza maswali, tuna miradi ya maji mingapi nchi hii? Tuna miradi ya barabara mingapi nchi hii? Tuna miradi ya umeme mingapi nchi hii? Yote hii inakwenda kwa Kamshina *General*.

Mheshimiwa Spika, utaona mchakato wa manunuzi *(procurement process),* kuna baadhi ya miradi inachukua miezi mitatu mpaka sita. Maoni yangu kwa Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Wizara, sioni kama kuna changamoto kama Kamishna *General* atakasimu majukumu yake kwa Mameneja wa *TRA* wa mikoa kwamba misamaha hii ya kodi ya ongezeko la thamani kwenye miradi yetu,

ikifanywa hivyo miradi itakwenda kwa kasi sana. Nimeona eneo hili nitoe mchango wangu na nimekuwa nikisema mara kwa mara jambo hili ni la kikanuni tu.

Mheshimiwa Spika, ukisoma Sheria yenyewe inaeleza tu, kuna sehemu hiyo ambayo Waziri anaweza akatoa fursa hiyo, na Kamishna wa *General* wa *TRA* akakasimu majukumu yake kwenye ngazi za mikoa, Mameneja wa Mikoa wa *TRA* wapewe mamlaka ya kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa miradi yote inayoombewa.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwa dhati, inayoomba hiyo kodi ya ongezeko la thamani, siyo Mkandarasi, anayeomba ni taasisi ya Serikali. Kwa hiyo, anaomba ni taasisi ya Serikali, *TRA* ni taasisi ya Serikali, hakuna mazingira ya rushwa hapo. Sasa sioni kwanini Kamishna Mkuu wa *TRA* asikasimu majukumu haya kwenye *level* za mikoa.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine nijielekeze pia kwenye eneo la Sheria ya Ardhi ukurasa wa 15, Marekebisho ya Sheria ya Ardhi, imeeleza kwa habari ya mlipa kodi ya ardhi, akichelewa kulipa ardhi kwa miezi sita kuna takwa la kutozwa riba ya asilimia 0.5 na miezi sita ijayo ni asilimia moja.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo lingine, ni maoni yangu eneo hili; kuna kodi nyingine ya ongezeko la mtaji, yaani *capital gain tax. Capital gain tax* ni asilimia 10. Nitoe tu mfano, mathalani; Mtanzania ameuza nyumba yake Shilingi Bilioni moja. Ukifanya hesabu ya kutafuta *capital gain tax,* yaani kodi ya ongezeko la mtaji, unapata *almost* Shilingi milioni 100. Hivi ni nani mwaminifu huyu akabeba fedha zote Shilingi milioni 100 anapeleka Serikalini?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kinachofanyika tunatengeneza mazingira ya rushwa kwa watendaji wetu wa TRA. Kwa hiyo, wote wanajadiliana tu katika namna ya kupunguza kodi. Na mimi niseme tu tunapoteza mapato

makubwa sana kwenye tozo hii, asilimia 10 ni kubwa sana. Maoni yangu na ushauri wangu ije walau asilimia tano, itarahisisha na mlipa kodi atakuwa rafiki ataenda mwenyewe kuweka fedha hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine na eneo langu la mwisho ni kuhusu marekebisho ya sheria za Serikali za Mitaa sura namba 287 na sura namba 288, narejea ukurasa wa 15 pia. Imeelezwa hapa kwamba marekebisho haya yanalenga kuanzisha vituo vya utoaji huduma vya pamoja *(One Stop Business center)*. Sasa hili jambo pia ni muhimu.

Mheshimiwa Spika, nashauri, ukiangalia miundo ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa; halmashauri za miji na halmashauri za wilaya; wana idara ya biashara. Tukianzisha vituo hivi, na tusiishie kuanzisha tu; ushauri wangu, kuwe na Afisa maalum anayeshughulika na masuala ya machinga. Kwa sababu machinga ni kundi kubwa na kundi muhimu. Kwa hiyo, Afisa huyo atasaidia kuratibu shughuli zote za machinga. Na faida yake ni nini? Tutajua idadi ya machinga ya eneo husika na hatuishii kujua tu, machinga anapaswa a-*graduate*.

Mheshimiwa Spika, sasa, tukianzisha vituo hivi vya biashara za pamoja kwenye halmashauri zetu na vituo hivyo vikawa na Maafisa wanaoshughulika, kwenye kanuni najua Waziri wa TAMISEMI yupo kwenye muundo wa kanuni kwa sababu kuna sehemu inampa mamlaka ya kuunda kanuni; Kwenye kanuni ni muhimu kwenye vituo hivi kukawa na Maafisa wanaoshughulika na wamachinga. Lengo letu wamachinga wa-*graduate* ili hatimaye nao wawe wafanyabiashara wakubwa. Na hii itasaidia kodi kwenye Taifa letu lakini kuongeza na ustawi wa Taifa letu kwenye mapinduzi ya uchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa leo michango yangu ni hiyo. Ahsante sana na Mungu akubariki. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Cecil David Mwambe atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota. Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina ajiandae.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, na mimi nikushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuchangia na kutoa mawazo yangu kwa nia ya kutaka kuishauri Serikali kufanya marekebisho ya baadhi ya sheria.

Mheshimiwa Spika, la kwanza kabisa nataka tuangalie kwenye ukurasa wa saba.

**SPIKA:** Ukitutajia kifungu utatusaidia zaidi kuliko ukurasa.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, sawa. Ukurasa wa saba *Cap. 203 part 5.* Hii ni sheria ya korosho; na nime-*move schedule of amendment;* kwenye sheria hii wanataka kufanya marekebisho lakini wanatumia sheria iliyopita. Sheria iliyopita ilikuwa inataka fedha zinazokatwa au zinazopatikana kutokana na makusanyo ya *export levy* asilimia 65 ya fedha ile ilikuwa inarudi kwenda kusaidia wakulima.

Mheshimiwa Spika, miaka ya hapo nyuma kidogo fedha hii iliondolewa yote kabisa na ikaenda Serikali Kuu. Juhudi kubwa sana zimefanyika kwa kushirikiana na Serikali na sisi Wabunge wote tunaotokea kwenye maeneo yanayolima korosho na tukapata mafanikio makubwa fedha ile ilirejeshwa. Na mwaka huu ikaanza kutumika kwa maana ya kupeleka ruzuku kwenye pembejeo ambazo zimesababisha wakulima kupewa pembejeo bure.

Mheshimiwa Spika, sasa Wizara ya Fedha inakusudia kufanya mabadiliko, na katika mabadiliko haya wameleta mapendekezo kwenye kifungu a, wanasema asilimia 50 itakuwa *remitted to the Ministries responsible for agriculture* kwa ajili ya kusaidia kwenye *subsides* za mazao. Lakini sisi

tunataka tuombe zaidi. Hii sheria itamke kabisa kwamba fedha hii inakwenda kutumika kwenye korosho kwa sababu ndiko inakokusanywa. Kwa hiyo, wakubali kuongeza hiki kipengele kama ambavyo iko kwenye *schedule of amendment* kwamba fedha hii ikatumike kwenye kuboresha au hizo *agricultural subsidies* kwenye zao la korosho kwa sababu ndiko inakokatwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kipengele cha pili tunaomba kiboreshwe na tunapendekeza iwe kama ifuatavyo. Kwanza tunaridhika kwa makato haya yanayofanyika. Isipokuwa sasa Serikali fedha inayokwenda kwenye *Agriculture Development Fund* iwe asilimia 15. Maana yake iwe *specifically* hapa ulifafanua tu wameweka tu asilimia 50 *as a block figure* kwamba asilimia 50 *shall be remitted to the Consolidated Fund.*

Mheshimiwa Spika, tunaomba iwe asilimia 15 iende kwenye *ADF (Agriculture Development Fund)* na asilimia 35 iende kutumika kwenye *Consolidated Fund* kama ilivyo, kwa maana ya kutaka kuchangia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, lakini tunapendekeza *in the future* basi na mazao mengine ambayo yanakuwa *exported* kutoka Tanzania na wenyewe wawekewe *export levy.* Kwa sababu makusudi ya hii sheria ilikuwa ni kutaka kuhakikisha badala ya ku-*export process* za haya mazao yafanyike nchini kwa maana ya kutaka ku-*create* ajira, kutaka kuzalisha ajira nyingi zaidi. Sasa wakawa wanaweka hizo fedha za *export levy* kama ni sehemu ya kukatisha tamaa watu wanaotaka ku-*export* na kuwa-*encourage* wajenge viwanda nchini kwetu. Lakini sasa hivi inatumika kama mapato na sisi tunakubali na tunanufaika nayo na tunaomba iendelee kama ilivyo kwa maana ya asilimia 50.

Mheshimiwa Spika, lakini iende sasa Wizara ya Kilimo kwa ajili ya kwenda kusaidia na hasa zaidi kwenye zao la

korosho kwa sababu mapato haya yametokana na mapato yanayotokana na korosho na siyo mapato ya mazao yote mtambuka. Kwa hiyo, iwe *specific* na sheria iseme wazi kwamba itasaidia kusaidia kwenye zao la korosho, kwa maana ya mikoa yote waliyoamua kufanya ukulima wa korosho ikawasaidie. Lakini hatutegemei tuone fedha hii inakwenda kusaidia kwenye karanga, inakwenda kusaidia kwenye ufuta sijui, inakwenda kusaidia kwenye mazao mengine. Ni maeneo yale tu iwe *specific* yanayolima korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na hii sehemu ya pili na yenyewe ikawe waziwazi kabisa, maana hapa wameweka tu asilimia 50 moja kwa moja iende Mfuko Mkuu. Tunatamani hii asilimia 50 iende kwenye kusaidia hizo *agricultural inputs* za korosho. Hii asilimia 50 igawanywe mara mbili, 15 iende kwenye *ADF* kwa maana ya sisi wakulima wa korosho tunaamua kwenda kuchangia Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo kwa asilimia 15. Halafu asilimia 35 inayobakia yenyewe iende moja kwa moja kuchangia kwenye *Consolidated Fund;* kwa maana ya Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya maendeleo ya nchi nzima ili tuweze kukamilisha kule kwetu ujenzi wa barabara Mtwara, Mlivata, Masasi, Nachingwea na huko kwingine kote ili tuweze kupata pale mazao mazuri pamoja na kuboresha bandari yetu.

Mheshimiwa Spika, sheria ya pili ambayo napenda nizungumzie ni sheria hii inayokusudia kuondoa tozo kwenye kuingiza mafuta nchini kwa maana ya ile asilimia 15. Wizara wameleta mapendekezo, wanasema kwamba sasa hivi…

**SPIKA:** Sasa kwa sababu wewe umetuongoza vizuri, kifungu cha ngapi?

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, hii *document* ni kubwa kidogo nimesahau kuandika hapa

kifungu lakini unaweza kunisaidia kama kiko karibu na wewe hapo au Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

**SPIKA:** Ni sheria gani?

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, sheria itakayokuwa inasaidia ku-*import crude oil.*

**SPIKA:** Sheria gani?

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya sheria kwa maana ya inayoondoa kodi kwenye *importation* ya *crude oil.*

**SPIKA:** Haya, endelea na mchango wako.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninachoishauri Serikali. Serikali inapendekeza waweke *zero rate,* kutoka asilimia 25 iliyokuwa inatozwa mwanzoni kwenye kuingiza *crude oil* nchini. Wana lengo zuri kabisa ikiwa ni pamoja na kupunguza *inflation* pamoja na kusaidia kwenye bei ya mafuta ili yasipande, kupunguza *inflation* kutoka asilimia 25 wameondoa *import duty up to zero* kwenye *crude oil.*

Mheshimiwa Spika, lakini nataka niwakumbushe Wizara wafahamu kwamba mafuta mengi tunayotumia hapa nchini kwetu yanatoka nje, na nchi nyingi ambazo tunachukua mafuta kwao hawaruhusu kuondoa *crude oil.* Kwa sababu wanapoondoa *crude oil* kule kwao na ku-*export* tafsiri yake wanapunguza ajira. Kwa hiyo, wanaleta mafuta ambayo yako *semi processed.*

Mheshimiwa Spika, sasa Tanzania sisi tuna viwanda na tunaipeleka nchi yetu kwenda kuwa nchi ya viwanda. Kuna viwanda vinavyofanya *processing* za mafuta ya kupikia. Sisi tulipata safari ya tukatembelea kiwanda kimoja Dar es

Salaam, *Murzah Oil* pale. Wao wanachokifanya kikubwa wanaanza kutoka *stage* za chini kwa kununua alizeti; na tunafahamu wazalishaji wengi wanafanya hivyo; baadaye wanakwenda ku-*process* alizeti wanapata mashudu, wanauza mashudu na mengine yanakwenda kutumika kwa mifugo na kufanya shughuli mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunapoamua kuondoa na kuruhusu watu wayalete mafuta nchini yakiwa *semi processed* kama ilivyo kwenye viwanda vya bati na vingine tunakuwa tumeondoa sehemu ya ajira, yaani tunapunguza. Hakuna mtu utakayemwambia aendelee ku-*maintain* wafanyakazi wanaokamua alizeti ilhali anafahamu akiingiza mafuta kutoka nje na kuyaleta hapa yakafikia hapa Tanzania kwa ajili ya kusafisha tu kidogo lakini baadaye kuyafanyia *packaging*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, watu wengi watakuwa wanakimbilia kwenye viwanda vya kufanya *packaging* pamoja na kuyapeleka mafuta sokoni, tutaondoa ajira, tutapoteza ile kodi ya *pay as you earn* pamoja na kodi nyingine. Kwa hiyo, nikuombe, na niiombe Wizara wazingatie hili. Kwa sababu tukifanya hivi hatutakuwa tena nia ya kulinda viwanda, tutaua viwanda vyetu na pia tutairudisha Tanzania kuwa kama nchi ya wachuuzi; kwa sababu wachuuzi ndiyo wale wanaoleta *either processed products* au *semi processed products.*

Mheshimiwa Spika, tuliona kwenye viwanda vya bati, wakati nilipochangia kama Mjumbe wa Kamati ya Viwanda na Biashara. Tulipata ziara ya kutembelea kwenye viwanda vya mabati, nao walikuwa wanalalamika kwamba kuna viwanda vinavyo *export* mabati kutoka nchi nyingine ambayo yamebakisha labda *process* mbili tu; kuyakamilisha ili yaweze kuingia sokoni. Na *process* mbili ni kuyapiga rangi pamoja na kuyawekea migongo na ya tatu ni kufanya *cutting*.

Mheshimiwa Spika, na uwezi kulinganisha bei za watu wanaoleta hayo mabati yakiwa tayari. Na nilitoa mfano hapa, ukiwa njiani unaweza ukapishana na yale malori yanayobeba zile *rollers* zinazokwenda kwenye viwanda. Utakuwa roli zingine zimebeba *rollers* sita mpaka nane kwenye gari la futi 40. Tafsiri yake ni kwamba wale wanayapeleka kwenye viwanda vya kupiga rangi, kuweka migongo pamoja na kukata. Kwa hiyo, unaweza ukakuta kuna wafanyakazi 10 wanaendesha mashine na bati zikatoka nje zikauzwa.

Mheshimiwa Spika, ukikuta gari imebeba *rollers* mbili ama tatu zile za futi 40. Tafsiri yake wanapeleka kwenye viwanda ambavyo vinaanza kurekebisha *size* na mengine.

Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa nafasi hii uliyonipatia na mimi naomba kutoa mchango wangu na Serikali ifanye marekebisho kama nilivyoomba, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota atafuatiwa na Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina. Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika ajiandae.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi ya kuchangia Muswada huu wa Fedha.

Mheshimiwa Spika, mimi nitajielekeza sehemu ya tano ambayo inazungumzia mabadiliko atakayofanya kwenye sheria ya tasnia ya korosho.

Mheshimiwa Spika, nataka nikurejeshe kule nyuma ambapo kabla hatujafanya mabadiliko ya 2017/2018 sehemu hii tulikuwa na sheria ambayo ilikuwa inatamka wazi kwamba fedha ambazo zitakusanywa kwenye *export levy* asilimia 65 ilikuwa inakwenda kwa ajili ya kuendeleza zao la korosho na

asilimia 35 ilikuwa inakwenda Mfuko Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza niipongeze Serikali kwa uamuzi huu wa kurejesha hii asilimia 50 kwa sababu ilikuwa ishaondolewa kabisa. Lakini nipongeze kwa hatua iliyofikiwa sasa hivi ambayo sasa tuna asilimia 50 inaenda Wizarani kwa ajili ya kuendeleza zao la korosho kupitia Mfuko wa *ADF* na asilimia 50 itakwenda kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni huu, kwamba zao la korosho linahitaji uwekezaji mkubwa sana. Utafiti ambao umefanywa na TARI - Naliendele unaelezea wazi kwamba kukiwa na ongezeko la matumizi ya pembejeo basi uzalishaji unaongezeka na mfano halisi ni msimu wa mwaka 2017/2018 ambapo Serikali ilithubutu kutoa tani 23,000 za *Sulphur* na tulifikisha tani 314,000, kiwango ambacho hatujawahi kufikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulivyoondoa hizi fedha za *export levy* uzalishaji uliporomoka kwa miaka mitatu. Lakini kwa mapenzi mema ya Mama, Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan alivyotoa pembejeo mwaka jana za korosho bure, mwaka jana uzalishaji uliongezeka kwa tani 40,000 na ndiyo maana tumefikia tani 240,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sehemu hii mimi naishauri Serikali kwamba, cha kwanza hizi fedha zisemwe kabisa *categorically,* kwamba zinakwenda Wizarani kwa ajili ya ununuzi wa pembejeo na shughuli zingine zinazohusiana na zao la korosho. Kama nilivyosema korosho inahitaji pembejeo, korosho inahitaji utafiti, korosho inahitaji kujiwekea malengo kwamba sasa tuingie kwenye ubanguaji. Kuna wabanguajia wadogo ambao wanahitaji kusaidiwa. Lakini korosho inahitaji usimamizi, Maafisa Ugani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Bashe alitoa pikipiki na vifaa vya kufanyia kazi kwa Maafisa Ugani. Sasa, tukipeleka hizi fedha za *export levy* kiasi kidogo basi wale Wagani wanaoshughulikia zao la korosho watafanya kazi kwa umakini zaidi na kwa ufanisi mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, korosho sasa hivi inazalishwa kwenye mikoa 17, na ndiyo maana tunaomba sasa kwamba hii asilimia 50 ieleze waziwazi kwamba inakwenda Wizara ya Kilimo lakini itaenda kwa shughuli za kilimo. Vilevile, kwa sababu kuna mfuko mpya huu wa kuendeleza kilimo *(ADF),* tunapendekeza sasa asilimia 15 nyingine itoke kwenye *export levy* ikapeleke kwenye mfuko huu mama ambao kama tulivyosema kwamba tunakusudia kwenda mapinduzi ya kilimo. Kwa hiyo, hapa mapendekezo ambayo ninaishauri Serikali ni kwamba turudi kwenye kiwango kilekile cha zamani asilimia 65, asilimia 60 iende kwenye korosho kwa maana pembejeo, utafiti na mambo mengine. Asilimia 15 iende kwa ajili ya Mfuko wa Kuendeleza Kilimo (*ADF)*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Chikota hebu tusaidie kidogo, kwa sababu ndiyo tuko tunaangalia hapa na hayo marekebisho yaliyopendekezwa. Hii *export levy* ni nani anayelipa? Ni mkulima au ni yule anayepeleka korosho nje? Nani anayelipa *export levy?*

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, *export levy* analipa mnunuzi lakini…

**SPIKA:** Ngoja ngoja, analipa mnunuzi wa korosho siyo mkulima?

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, mnunuzi wa korosho siyo mkulima.

**SPIKA:** Hiyo ni ngazi ya kwanza. Umesema hapo kwamba Mheshimiwa Rais mwaka jana alitoa *Sulphur* bure.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Hizo fedha zilitokana na *export levy* au hapana?

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, hapana hizo fedha ni kwa uamuzi wake tu kwamba anataka kutoa…

**SPIKA:** Ahaa hazikutokana na *export levy?*

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, haikutokana na *export levy*.

**SPIKA:** Haya ahsante.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, sasa nataka nitoe ufafanuzi hapo kwamba pamoja na kwamba anatoa mnunuzi, lakini mnunuzi anapokwenda sokoni anajua kwamba baadae atatoa kiasi kwa ajili ya *export levy* kwa hiyo, hata ile fedha ya sokoni anapunguza. Kwa hiyo, utakuta anayeathirika zaidi pale ni mkulima.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa sababu hiyo ninashauri, kwamba ukiwekeza fedha kwenye pembejeo basi uzalishaji utaongezeka na Serikali itapata fedha zaidi. Kwa hiyo, naomba hii asilimia 50 tuipeleke kwenye korosho, asilimia 15 tupeleke kwenye Mfuko wa Kuendeleza Kilimo (*ADF)* kwa hiyo, itakuwa jumla 65 na Mfuko Mkuu wa Serikali iende asilimia 35.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina atafuatiwa na Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika. Mheshimiwa Ali Hassan Omar King ajiandae.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii uliyonipa ili na mimi nichangie Muswada huu wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, awali kabisa ni yale maeneo ya marekebisho ya sheria ya marekebisho ya usimimizi wa kodi sura namba 438 ambako Wizara imekubaliana, Serikali imekubaliana na nimpongeze sana Waziri, Naibu Waziri na wataalam wake wote na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kukubaliana na ushauri wetu. Pamoja na hayo pia na yale marekebisho yaliyofanyika ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa kulinda zile fedha za wajasiriamali haya yote tunaipongeza Wizara ya Fedha kwa kukubaliana na sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nizungumzie Marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mapato Sura 332 pamoja na Kodi ya Ongezeko la Thamani Sura 148, ambapo katika eneo hili Waziri wa Fedha anapewa mamlaka ya kusamehe kodi ya ongezeko la thamani na pia kusamehe kodi ya mapato ya wawekezaji mahiri maalum baada ya kupata ridhaa ya Baraza la Mawaziri.

**SPIKA:** Nisaidie kifungu niwe nakitazama hapa Mheshimiwa.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, kifungu hapa ni 127 kwenye kodi ya ongezeko la thamani.

**SPIKA:** Sawa endelea.

Mheshimiwa Spika, kifungu 127 ambapo Waziri anapewa mamlaka ya kusamehe kodi kwa wawekezaji mahiri, maalum, baada ya kupata ridhaa ya Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, kama Kifungu hiki kitapita hivi kilivyo kina changamoto kubwa. Moja ni kumuingiza Mheshimiwa Rais katika mchakato wa usameheaji wa kodi na tunajua madhara ya kumuingiza Mheshimiwa Rais katika mchakato wa kusamehe kodi. Inawekezakana kabisa Mheshimiwa Rais akashauriwa vibaya, tunapotunga sheria tusiangalie watendaji waliopo kwa sasa au uongozi uliopo leo, anaweza Mheshimiwa Rais akashauriwa vibaya akaenda kuingia misamaha ya kodi ambayo imejaa upendeleo, ambayo ni rushwa, ambayo imesababishwa na ufisadi ndiyo msamaha ule ukatokea, endapo ikifanyika hivyo maana yake Serikali nzima itakumbwa na kashfa.

Mheshimiwa Spika, sasa Serikali nzima ikikumbwa na kashfa ya rushwa na ufisadi tutaweka wapi macho yetu? Lakini kwa nini Kiongozi wetu Mkuu tumuweke kwenye mambo *operational* namna hii, na kwa kufanya hivi pia itakuwa pia ni kama kumkingia kifua Waziri wa Fedha ambae atafanya maamuzi mabaya kwa kinga ya kwamba amepita kwenye Baraza la Mawaziri na amemwingiza Mheshimiwa Rais, hivyo, nadhani hii si sawa.

Mheshimiwa Spika, jambo la Pili kama nilivyosema wakati ule nachangia kwamba, kwa nini uwe na misamaha ya kodi ya *group* la watu, la mtu mmoja mmoja kwa kutambulika kwamba ni mwekezaji mahiri, kwa kutambulika kwamba huyu anakuja kuwekeza, hali hii itaondoa ushindani wa haki, kwa sababu kujua kwamba huyu ni mwekezaji mahiri na kujua kwamba huyu anastahili kupewa hii misamaha, tutaenda kuingia huko huko ambako watu wengine watasamehewa kodi, wengine hawatasamehewa kodi lakini wanaenda kushindana kwenye sekta moja. Kwa hiyo, suala hili linaweza kutuletea madhara makubwa sana, kuna viwanda vingine vitafungwa na kuna wengine watashindwa kushindana kwa sababu wenzao wamepata msamaha.

Mheshimiwa Spika, jambo la Tatu katika eneo hili, wawekezaji hawa hawatavutwa na misamaha ya kodi pekee. Misamaha ya kodi nafasi ndogo sana ya kuwavuta wawekezaji kuja kuwekeza kwenye nchi yetu, tupambane tuwezavyo ndani ya nchi yetu vivutio vikubwa ni kuhakikisha kwamba tuna bandari ambayo inafanyakazi kwa ufanisi, tupambane tuwezavyo tuhakikishe *SGR* yetu imekamilika, tupambane tuwezavyo tuhakikishe kwamba tuna umeme wa uhakika na wa bei nafuu, tupambane tuwezavyo tuhakikishe kwamba *infrastructure* za uchumi zote zimeimarishwa na zimeboreshwa vizuri, wawekezaji watakuja hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo mimi napendekeza kabisa kwamba hili eneo la kupendelea baadhi ya watu hata kama ingekuwa ni miradi ya kimkakati tunaitungia sheria, kama ni miradi ya kimkakati isingeandikwa mwekezaji mahiri, ingeandikwa kama ni *project* za hapa nchini tunazozisamehe kwa sababu, kwa mfano bomba la mafuta lile la Uganda kama tunalisamehe lile linaletwa Bungeni kwa mchakato wa kupitia kwenye kamati zetu halafu tunatoa msamaha, lakini ikiletwa namna hii tunaenda kukwamisha mapato ya Serikali, watu wengine watatumia *room* hii kutengeneza ufisadi na rushwa na mwisho wa siku tutakosa mapato na mwisho wa siku tutauwa uchumi nchini.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ninalotaka kulizungumza wenzangu wamezungumzia hili suala la korosho hiki kifungu cha 17A katika Sheria ya Korosho Sura ya 18. Ilivyowekwa pale haieleweki vizuri.

Mheshimiwa Spika, unasema kwamba unapeleka fedha asilimia 50 amezungumza jirani yangu hapa Mheshimiwa Chikota, unapeleka asilimia 50 Wizara ya Kilimo halafu unapeleka Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo, halafu husemi Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo zinapelekwa *percent* ngapi, na husemi Wizara ya Kilimo yenyewe inapelekewa shilingi ngapi.

Mheshimiwa Spika, pili eneo hili kama sheria itapitishwa kama ilivyo itavunja sheria zingine, tulishakubaliana hapa kwamba Wizara zote haziwezi kubaki na *retention,* kwa hiyo kwa jinsi sheria ilivyo maana yake unataka kusema *TRA* wakusanye fedha, wazitume moja kwa moja kuja Wizara ya Kilimo. Sasa hili limekaaje kwa sababu *retention* zote tulishaziondoa kwenye Wizara! Kama tulitaka hivyo, kwa maana hiyo hiyo bila kuondoa maana wala kurekebisha matumizi ya fedha hizo, fedha hizo zingeenda kwenye Mfuko Maalum kwa maelekezo ya matumizi yanayopendekezwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, siyo fedha ziende tena Wizara ya Kilimo, Wizara ya Kilimo unaipelekeaje fedha kutoka kwa mkusanyaji? Haiwezekani na sheria hairuhusu.

Mheshimiwa Spika, lingine kwa Waziri wa Fedha katika eneo hili ni la kumuuliza kwamba, kwa nini ni zao la Korosho tu, mazao mengi yanayolipa *export levy* mifugo inalipa *export levy* kila leo, nyama, maziwa tunapouza Wanyama Hai, tunapouza Mazao ya Uvuvi tunalipa *export levy,* kwa nini *export levy* hakuna kinachobaki kwa ajili ya wavuvi kwa nini ni korosho tu peke yake korosho tu katika eneo hili?

Mheshimiwa Spika, kama nia njema ya Serikali ilikuwa kuyaendeleza haya mazao, kwa nini mazao yote *export levy* isingeweza kurudi kwa ajili ya wazalishaji, Mifugo wakapata Wavuvi wakapata wazalishaji wa Tumbaku wakapata, wazalishaji wa Kahawa wakapata kwa nini? Kwa nini….

**SPIKA:** Ngoja Mheshimiwa, hayo unayoyasema yapo kwenye marekebisho, Serikali haijasema hizo pesa zitaenda kwenye korosho, kwenye hii ninayoitazama hapa Serikali haijasema *export levy* inayotokana na korosho itaenda kwenye korosho ahh! Ni marekebisho yaliyoletwa na Mheshimiwa Cecil Mwambe ndiyo yanatakana kwamba

sheria iseme sehemu ya hiyo *export levy* itaenda kwenye korosho.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, kwa vyovyote vile itakavyokuwa, hizi fedha kama zinaletwa kwa ajili kuboresha kilimo, maneno aliyoyatumia Waziri wa Fedha ni mazuri sana kwamba ni kwenda kuboresha kilimo, sasa kama ni hivyo, hata kama haziendi kwenye korosho pekee, *concern* yangu hivyo hivyo kama shabaha sasa ni kwa ajili ya kuanza kuziendeleza sekta zinazozalisha mazao haya, kwa nini mazao mengine yameachwa ili kuongeza hata huo mfuko ziende kwenye mifugo, ziende kwenye uvuvi, ziende kwenye mazao mengine.

**SPIKA:** Sasa hilo ndiyo lilikuwa kazi yetu sisi Bunge hapa, yaani marekebisho hayo yalitakiwa yawekwe hapa mbele Mheshimiwa Mpina, yaani uwe umeleta kwamba kwa nilivyoona hii sheria inavyorekebishwa na hizi sheria nyingine turekebishe kwa pamoja Serikali ili tuenda vizuri, ndiyo kazi yetu sisi hiyo.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, umepotia asilimia 100 na kwa kweli hata sitaki kurudia maneno uliyoyasema ndicho hicho hasa tunachotaka hapa kifanyike, kwa ajili ya kuweza kuimarisha kilimo chetu nchini.

Mheshimiwa Spika, pendekezo lingine ni Sheria ya Bima, Sura 394, Kifungu Kipya cha 133 ambacho kinazungumzia suala la bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ya nchi na zenyewe zikatie bima. Hapa kuna changamoto, unasema bidhaa zote zinazotoka nje zikatiwe bima, chombo cha usafiri kinachotumika kusafirisha mazao haya kuyaleta hapa nchini kimekatiwa bima, *storage* zote zinazotumika kwa ajili ya kutunza haya mazao zimekatiwa bima, unataka na mazao yenyewe yakatiwe bima kwa ajili ya nini?

Mheshimiwa Spika, hii siyo ni kuongeza gharama kwa walaji bila sababu yoyote? Unayakatia bima ili ufanye nini na hili kama litapita hivi lilivyo tunaenda ku-*support* mfumuko wa bei unaoendelea hapa nchini kwa sababu mwisho wa siku tutakaoenda kuwaadhibu ni wale wanaotumia mazao hayo.

Mheshimiwa Spika, ninashauri kwa sababu tumependekeza vizuri mambo mengine lakini hili eneo la bidhaa zinazoagizwa kutoka nje nchi ziondolewe kwenye ulazima wa kukatiwa bima, hii itakuwa ni *double standard* na tutakuwa tunaongeza gharama za wananchi wetu bila sababu yoyote ile ya msingi.

Mheshimiwa Spika, pia tumependekeza kwamba masoko na minada yote iweze kukatiwa bima, hasa ni lazima hapa pia tuangalie tunatoa mapendekezo haya ikiwa Bajeti za Serikali za Mitaa tayari zimekwisha kupitishwa na haijulikani kiwango gani cha fedha kitahitajika kwenye eneo hili, kwa hiyo tunaweza tukapeleka huu ulazima ukaenda kuharibu bajeti zote tulizozipitisha za Serikali za Mitaa kwa ajili ya gharama kubwa ya kulipia hizi bima.

Mheshimiwa Spika, sasa ushauri wangu katika suala la masoko na minada, najua tumeshapata hasara nyingi masoko yameungua wananchi wetu hawajaweza kufidiwa ni jambo ambalo ni la lazima kwa sasa, lakini lifanyike katika namna ambayo haitaenda kuvuruga bajeti tulizokwisha kuzipitisha katika eneo hilo la Serikali za Mitaa. Pendekezo la pili ni kwamba bidhaa zote za kutoka nje ya nchi ziondolewe kwenye bima ya lazima.

Mheshimiwa Spika, baada ya kumaliza kupitia haya maeneo ambayo ni *specific* ya kisheria, nataka kuona tu kwamba jinsi *Finance Bill* inavyopitishwa. Historia huwa inajirudia tulikuwa na makosa mengi sana kule nyuma ya upitishaji wa bajeti lakini Mama shupavu Mama Anna Semamba Makinda Spika wa Bunge la 10 aliweza kufanya

mabadiliko haya, tulikuwa tunapitisha na bajeti halafu baadaye tunaanza kujadili Wizara na baadaye tukitoka Wizara tulikuwa tunapitisha bajeti, tukimaliza tu kuipitisha tu bajeti tunaanza kujadili Wizara, halafu baadaye ndiyo tunaenda kumalizia na *Finance Bill*.

Mheshimiwa Spika, hatukuwa na Kamati ya Bajeti wakati huo tukafanya mabadiliko, haya yote yakawezekana, leo hii tumemaliza kupiga kura ya kupitisha bajeti ya Serikali lakini *Finance Bill* ikiwa haijapita, maana yake tumeipitisha bajeti ya Serikali kukiwa hatujakubaliana eneo la mapato, maana yake Bunge lako limeshiriki kupitisha bajeti ambayo kwa sehemu kubwa haijaikubali bajeti hiyo, na tumepiga kura ya kila mmoja *Finance Bill* hatujajadiliana kukubaliana, nadhani haya ni mapungufu makubwa katika mfumo wa upitishaji wa bajeti.

**SPIKA:** Sawa. Sasa Mheshimiwa Mpina muda wako umeisha, kwa mawazo yako tunatakiwa kupitisha kwanza sheria kabla ya kupitisha bajeti.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, kwa mawazo yangu mimi tukamilishe mambo yote, *Finance Bill* ikamilike, *Appropriation Act* kama tulivyoikamilisha, halafu sasa tunapiga kura.

Mheshimiwa Spika, mimi kwa umakini huo huo kama nilivyosema historia huwa inajirudia, kwa ushupavu wako na umakini ulionao na usikivu wako, naamini hili utalifanyia marekebisho ili Bunge letu liweze kupiga hatua kubwa katika maamuzi.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu huwezi ukapitisha bajeti ukapiga kura halafu kumbe eneo la mapato lote hujakubaliana nalo, inafika leo una- *criticize* mapato ambayo umeshayapigia kura tayari, kwa maana hiyo hata mapato yenyewe unaingia kwenye *deficit budget* hata kabla ya

bajeti yenyewe haijaanza, hivyo utaratibu huu ukiubadilisha utaweka historia katika nchi yetu na tutaenda vizuri zaidi, ahsante sana.

**SPIKA:** Umeeleweka Mheshimiwa.

Waheshimiwa Wabunge, ndiyo maana nasema hivi, nirejee tena ngazi hii tunatunga sheria kwenye kitu ambacho tunacho tayari, ndiyo maana ngazi hii hutakiwi kuleta jambo jipya kwa sababu hakuna mahali pakuliweka. Hata kama unayo mawazo yako ngazi hii hata ukiyaleta humu hayaingii. Hayaingii siyo kwamba kuna kosa la mtu mahali hapana! Hayaingii kwa sababu ngazi hii tunatunga sheria na sheria tulishaletewa, ilibidi tuwe tunaitazama hii wakati tunatazama na mengine. Kwa hiyo, haiwezekana ngazi hii tukaanza kuona kwamba hii sheria iliyoletwa haiendani na kile tulichopitisha hapana. Kile tulichopitisha tunakiwekea misingi kwenye sheria ili Serikali ikafanye hicho.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo tunaenda ngazi kwa ngazi, sijui tumeelewana? Nadhani tumeelewana ndiyo maana ngazi hii inabidi uje hapa na Kifungu wewe unasemaje na uwe umeleta marekebisho kwa sababu tumeshafika mwisho huku, kama hujaleta marekebisho halafu una mawazo yako, yaani hayo mawazo yako hata Waziri hapa mbele haji kuyajibu labda awe na muda mwingi ndiyo atajibu. Atajibu vifungu ambavyo tumependekeza mabadiliko.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo ngazi hii tuko kwenye kutunga sheria na kutunga sheria tunaangalia vifungu, yale tunayotaka yarekebishwe tulishapewa Sheria hii mapema, unakuwa umeshaleta. Hapa ninayo marekebisho ya Serikali ambayo wamekubaliana na Kamati na ninayo marekebisho ya Mbunge mmoja tu ambae yeye hajakubaliana na Kifungu kaleta marekebisho yake. Kwa hiyo

ngazi hii siyo ngazi ya mawazo mapya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika atafuatiwa na Mheshimwa Ali Hassan Omar King Mheshimiwa Leah Komanya ajiandae.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi na maelezo uliyoyatoa sasa hivi yananiweka katika ngumu zaidi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sina mawazo mapya lakini mawazo nilikuwa nimeshayatoa nikiwa na matumini yangekuwa yamejumuishwa katika sheria. Kwa maana ya mabadiliko lakini nitaongea kwa kifupi na kwa ujumla tu, kwa sababu bado nadhani ni mambo ambayo Mwenyekiti wetu wa Bajeti na Kamati yetu ya Bajeti imelisisitiza sana.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu na bajeti hii tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwamba imekwenda kuanza kuangalia namna gani inaweza ikaondoa matatizo na ikafanya ile *blue print* ianze kufanyika katika maeneo mbalimbali, kwenye kilimo na kwenye viwanda na hasa kwenye kulinda viwanda vyetu, kwa hiyo, kuna hatua nyingi za kikodi zimefanyika.

Mheshimiwa Spika, wakati nachangia niliongea wakati ule kwamba kwenye viwanda vya chuma bado kuna tatizo, nilikuwa nimetegemea labda lingesikika na sikuona mapema labda ningeweza kulileta lakini nitaliongelea kwa haraka tu.

Mheshimiwa Spika, bado tuna tatizo ukiangalia kwenye *HS code* zimewekwa sasa hivi *HS code* 9406.2090 ambayo kimsingi inaongelea *pre-fabricated designs,* sasa hivi imewekewa *zero rate*.

Mheshimiwa Spika, nilisema wakati ule na ninasema tena kwa kifupi kwamba kwa kuweka *zero rate* kwenye *pre-fabricated designs* za *materials*, *buildings* tumewaweka katika *disadvantage* viwanda vya ndani kwa sababu wao bado wanaagiza *material* kwa ajili ya kutengeneza hizo *designs* mbalimbali za *pre-fab* na matokeo yake ni kwamba itakuwa ni *cheaper* kwa mtu kuagiza kitu ambacho kimeshakuwa *molded,* kimeshatengenezwa kukileta nchini, wakati kingeweza kufanyika hapa.

Mheshimiwa Spika, tuna viwanda vya chuma *capacity* ni kama asilimia 40 tu ya uzalishaji vingeweza vikafanya kazi hapa vika-*design* na vikajenga, kwa kufanya hii kitu tunajikoshesha sisi kwanza mapato lakini cha pili tunaua ajira. Ninafikiria kwa mbele basi waliangalie kwa makini sana hili jambo.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili kwenye Muswada wa Sheria uliyopo mbele yetu ya Wakala wa Meli, Sura 415, tunamshukuru Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri kwa kufanya maamuzi ambayo kwa muda mrefu yamekuwa ni magumu kufanyika na sasa wameyafanya katika Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kuondoa *mandate* ya *TASAC* kufanya kazi kwenye maeneo fulani Fulani, sasa wameacha maeneo matatu tu, kutoa mizigo yote inayohusiana ambayo ni silaha, makinikia na nyara za Serikali.

Mheshimiwa Spika, sasa kuna suala la msingi hapa ambalo ni kwamba kwa sheria za nchi yetu tumekuwa tukiangalia viwanda vya *cement* kama vile ni viwanda vya uzalishaji wa madini, hilo jambo limepelekea sasa hata kwenye utunzi wa sheria na utaratibu wa sheria kwamba baadhi ya vitu ambavyo visingetakiwa viwe katika sekta hii ya uzalishaji wa *cement* tunaviingiza kama vile vipo katika madini.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kusema kwamba kwenye *HS Code* 2523 ambayo mimi nilidhania ingetolewa, haikutolewa baada ya Serikali kuwa imeridhia kulimiti *mandate* ya *TASAC,* unakuta bado vitu kama *clinker* ambayo ni *raw material* kwenye *cement* bado itaendelea kuwa *cleared* na *TASAC*.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli jambo hili linaipa tu urasimu, linaongeza gharama kwenye viwanda vya *cement,* ni vizuri basi hata kama sikuleta mabadiliko liangaliwe kwa makini ili huko mbele nayo hii iondolewe kwa sababu haina uhusiano wowote na makinikia. Nadhani ni kosa tu la kiutaalam la muda mrefu, tungeiondoa hiyo ili na yenyewe isiwe sehemu ya makinikia na ifanyike katika utaratibu wa kawaida ili kuvipa *efficiency* viwanda vyetu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya atafuatiwa na Mheshimiwa Issa Mchungahela, Mheshimiwa Neema Gelard Mwandabila ajiandae.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kutoa mchango wangu katika hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Waziri wa Fedha kwa kuleta Muswada na kupokea maoni ya Kamati na kuweza kuyafanyia kazi, kwa hatua hii nampongeza sana.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kushukuru Serikali kwa kutofanya marekebisho ya kubadili mgawanyo wa asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, wewe mwenye ni shahidi kwa namna Wabunge wengi walivyokuwa wakiunga kwamba

asilimia 10 isifanyiwe mgawanyo hii inaonekana ni kwa kiasi gani fedha hii inawasaidia wananchi wetu, ni kiasi gani bado kuna uhitaji mkubwa wa vikundi kuweza kupata hii asilimia 10.

Mheshimiwa Spika, hapa nilitaka kushauri sasa ni wakati muafaka, ni fursa kwa mabenki yetu kuliona hili jambo la uhitaji wa mikopo kwa vikundi vyetu katika Halmashauri. Kwa kuwa sasa, kama kikundi kinaweza kukopa *Coaster* ya Shilingi Milioni 100 itashindwaje kukopeshwa na mabenki yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa changamoto ni mabenki yetu yaone uwezekano wa kupunguza masharti ikiwepo na vigezo pamoja na dhamana ya mkopo, ikiwezekana basi Wakurugenzi waweze kuwadhamini vikundi kama hivyo ili viweze ku-*graduate* viende kwenye mabenki viachie vikundi vidogovidogo vingine vinavyoweza kuchipikia, kwa sababu kila mwanachi, kila kijana anayo haki ya kuweza kupata mkopo huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie Sheria ya Mifumo ya Malipo, Sura 437 na lengo la marekebisho ni kuweka usawa kwenye utozaji wa tozo hii kwenye miamala inayofanana. Ninaipongeza Serikali kwa kuchukua hatua hii kwa sababu mwaka jana tozo hizi ziliwekwa kwenye makampuni ya simu ambayo yaliwasababisha wananchi wengine kuhama na kwenda kwenye taasisi nyingine zinazofanya miamala kama hiyo. Kwa hiyo, iliathiri mapato ya makampuni ya simu, pia kodi ya pato kutoka katika makampuni haya. Kwa kufanya hivi, italeta usawa na Serikali ione iendelee kuangalia kodi za aina hii ziwezwe kutozwa kwa aina hii.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nishukuru kwa kuweka ukomo wa tozo ya shilingi 4,000 kutoka shilingi 10,000, hii itawapunguzia ugumu wananchi wetu kwa sababu wengi wanaotumia miamala hii ni wenye biashara ndogo ndogo,

lakini wenye kipato kidogo kidogo, lakini mitaji yao ilikuwa inaliwa kutokana na gharama kubwa iliyokuwa imewekwa. Nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kusikiliza jambo hili na lengo la Serikali pia ni kupanua wigo wa watu wengi kuweza kuchangia katika tozo hizi.

Mheshimiwa Spika, nikiri tozo za mwaka jana zimeweza kufanya makubwa katika Jimbo la Meatu tumejenga Kituo cha Afya Iramba Ndogo tumekamilisha madarasa katika Shule za Sekondari Bukundi, Mwamanongu na Ng'hoboko. Kwa hiyo, niwaombe wananchi kwa kuwa kiwango kimeteremshwa, naamini wengi watarudi kuweza kutumia huduma hizi ambazo wengi waliacha au kutumia mbadala wake.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee kuhusu Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura 41; Serikali imepunguza kiwango kwenye zawadi ya ushidi game task on winnings kutoka asilimia 15 hadi asilimia 10. Niishukuru Serikali ya Awamu ya Sita kwa usikivu wake kwa sababu tozo hii imeanza kupungua kutoka mwaka jana na hili lilikuwa ni ombi la *Gamming Board,* wakati inaanza 2015 ombi lake lilikuwa ni kutoza kwa asilimia 10, lakini Serikali iliweka asilimia 20 kwa wakati huo ilikuwa sawa na *VAT*.

Mheshimiwa Spika, kwa wakati huo, kodi hii ilikuwa ni kubwa, kwa hiyo ilileta mdololo katika kupatikana kwa mapato ya Serikali lakini ilileta mdololo katika mchezo mzima, kwa sababu Watanzania wengi walikuwa wanaenda kucheza michezo ya nje ambayo hawatozi kodi yoyote, kwa hiyo waliacha kucheza katika michezo ya ndani.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mheshimiwa Waziri, niishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kuendelea kupata, tunaona tulivyopunguza kutoka asilimia 20 mwaka jana hadi 15, kulikuwa na ongezeko la kodi ya bilioni 4.2 na hiyo ilikuwa ripoti hadi Aprili mwaka jana, lakini sasa na hivi

tunavyoendelea, Serikali itaendelea kupata zaidi kutokana na kupungua kwa tozo hii. Hili ni jambo pia la kujifunza kwa namna tunapoona kuna wigo mkubwa Serikali iendelee kupunguza tozo ili wananchi wengi waendelee ku-*comply* vizuri bila changamoto yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niipongeze Serikali kwa kuchukua hatua ya kuondoa hatua ya kutoza kodi ya awali kwenye kodi ya mapato ya shilingi 20 kwa kila lita ya mafuta pamoja na sababu zilizoelezwa na Serikali, lakini wauzaji wengi wa rejareja hawana mitaji, wanategemea kukopeshwa ndiyo waweze kulipa. Kwa hiyo tukiweka hii kodi wangeweza kuyumba katika biashara hii. Hii pia inasaidia kwa jicho la pili kwa sababu kila kulipo na vituo vya mafuta, mkoa una malengo yake ya kukusanya. Kwa hiyo, tukipeleka kwenye *pull* tutakosa jicho la pili la kuangalia kama kodi imeweza kulipa. Nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kuchukua hatua hii.

Mheshimiwa Spika, niongelee marekebisho kwenye Sheria ya Ardhi, Sura 113, nishukuru kwa hatua zilizochukuliwa, lengo likiwa kuhamasisha ulipaji kodi kwa hiari, lakini nataka niseme pamoja na marekebisho hayo yaliyofanywa, kodi nyingi zimelala kwenye hati ambazo zimeshikiliwa kwenye Ofisi za Makamishna zilizoko mikoani hata tukipunguza hii riba hakutakuwa na ufanisi kama Wizara haijachukua hatua ya kuwaambia maafisa kuziachia hati, hati za viwanja walizozishikilia katika maofisi. Ufike wakati kwa jinsi dunia inavyokwenda ya kidigitali, Wizara nayo sasa itumie mitandao kuwajulisha wananchi wanaomiliki viwanja sasa muda umefika wa kulipia. Kinachofanyika ni kusubiri kuletewa karatasi ama unapohitaji kuhusu kiwanja chako ukikenda pale ofisini ndiyo unaambiwa una deni.

Mheshimiwa Spika, nishukuru sana na niunge mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahante sana. Mheshimiwa Issa Mchungahela, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango ajiandae.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu. Pili, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii. Pia niishukuru Serikali, naomba nianze kuishukuru na kuipongeza Serikali kwa dhamira yake njema kwa wakulima wa korosho.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeleta mapendekezo ya mabadiliko ya Sheria ya Korosho, sheria namba 203, Sheria hii kabla ya mabadiliko ilikuwa ikielekeza kwamba kiasi cha *export levy* asilimia 65 kilikuwa kinakwenda kwenye Mfuko wa Bodi ya Korosho na asilimia 35 ilikuwa ikienda kwenye Mfuko Mkuu. Mwaka 2017/2018 kulitokea mabadiliko ambayo ililazimisha kwamba fedha yote ya *export levy* iende ikatumike kwenye Mfuko Mkuu hali ambayo kwa namna moja kulikuwa na changamoto kiasi kwenye uzalishaji lakini na uendeshaji wa zao la korosho.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kutuletea mabadiliko haya kwenye sheria namba 203, sheria ya sasa hivi inayopendekezwa, inapendekezwa kwamba asilimia 50 ziende kwenye Mfuko wa Wizara kwa ajili ya maendeleo ya kilimo, lakini asilimia 50 ielekezwe kwenye Mfuko Mkuu. Sasa ninayo mapendekezo kwenye sheria hii ili yafanyike mabadiliko na mabadiliko ninayoyapendekeza ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napendekeza asilimia 50 ipelekwe moja kwa moja katika Mfuko wa Bodi ya Korosho. Asilimia 15 ipelekwe kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo yaani kwenye Mfuko wa Wizara na asilimia 35 napendekeza ipelekwe kwenye Mfuko Mkuu. Kwa maana hivyo *export levy* itakuwa imefanya kazi nzuri sana ya kuchangia zao ambalo

ndiyo linazalisha lakini pia itakuwa imefanya asilimia 15 kwenye mchango wa mazao mengine kwenye kilimo na halikadhalika itakuwa imeichangia Serikali. Hapa tunaweza tukaona mgawanyo huu utakuwa ni mgawanyo wenye tija.

Mheshimiwa Spika, najaribu kusema hivi kwa sababu gani? Kwa sababu kwanza korosho ni miongoni mwa zao mkakati ambayo inailetea Taifa hili fedha nyingi sana za kigeni, lakini pia hali ya sasa ilivyo mikorosho peke yake ndiyo inayotozwa *export levy* na kiuhalisia hilivyo ni kwamba pamoja na kwamba export levy inalipwa na mfanyabiashara lakini yeye mfanyabiashara anafidia kwa kuweka bei ndogo kwa mkulima. Kwa hiyo mkulima anapunjika, baada ya kupata bei kubwa anapata bei ndogo kwa sababu ya ile *export levy*. Kwa hiyo ni busara kwamba fedha hii sasa ya *export levy* imguse yeye kwa kiwango kikubwa na kuhakikisha kwamba baadaye ana uwezo wa kuzalisha zaidi.

Mheshimiwa Spika, sababu nyingine kubwa ni kwamba, tumewekewa lengo kubwa la uzalishaji wa korosho. Sasa hivi lengo lililopo ni tani laki saba mpaka kufikia mwaka 2020/2025. Lengo hili hatuwezi kulifikia kama hakutakuwa na mkakati madhubuti wa kuifanya korosho iendelee. Njia pekee ya kuifanya korosho ni njia ya kuiwezesha kimapato hasahasa pato linaloweza kushughulikia kufanya utafiti. Utafiti hapa nazungumzia utafiti wa mbegu, utafiti wa magonjwa ya korosho, hali kadhalika na utafiti wa masoko. Mambo haya yote yataiwezesha korosho kuendelea na kwa sababu mkulima atakuwa *motivated* kuweza kulima kwa nguvu, mpaka hiyo *target* ya tani 700,000 inaweza kufikiwa kwa sababu atakuwa na uwezo wa kupata tija kwenye ukulima wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimejaribu kuzungumzia pia suala zima la maendeleo kwenye korosho, hapa tunazungumzia viuatilifu. Kwa mfano, mahitaji halisi ya korosho kwenye viuatilifu ni tani 45,000, lakini mpaka sasa hivi *commitment* ya

Serikali ni tani 25,000. Kwa bahati mbaya mpaka hivi tunavyoongea, hata nusu ya tani ambazo Serikali imetoa *commitment* bado hazijamfikia mkulima. Kipindi hiki ndicho kipindi halisi cha matumizi ya viatilifu sasa ndiyo kipindi ambacho mkulima anapuliza zile dawa kwa maana ya *sulphur* na dawa za maji.

Mheshimiwa Spika, sasa kama hata nusu ya dawa hizo hazijafika tunaweza tukaona hapo tatizo linaloweza likazalisha tatizo lingine. Kuepusha tatizo hili ndipo nilipopendekeza kwamba asilimia 50 iende moja kwa moja kwenye zao la korosho kupitia Mfuko wa Korosho iwe inashughulikia masuala haya ya viatilifu, lakini iwe inashughulikia na masuala mengine pia ya uendelezaji kama vile kuangalia jinsi gani labda tunaweza tukapata kuiongezea thamani korosho, lakini na shughuli nyingine zote zinazohusisha mnyororo mzima wa thamani ya korosho.

Mheshimiwa Spika, kwa kufanya hivi tutakuwa tumefanya jambo sahihi na tuna uhakika wa kupata mazao makubwa tuliyojipangia na maendeleo kwa ujumla kwa wakulima yatakuwa mazuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Said Issa, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamad Chande, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango na mtoa hoja, ajiandae.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hoja iliyopo mezani, Mmarekebisho ya Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, kwa kuanzia mchango wangu nitajielekeza kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato, *Cap. 332.*

Hapa sheria ambayo inataka kubadilishwa inakuja kuleta kodi ya mfuto, kodi ambayo kwa upande wa Zanzibar na bara itakuwa ni sawa. Hii kodi pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri wa Fedha atakuwa ameshauriana na Waziri wa Fedha wa Zanzibar, lakini bado suala hili utekelezaji wake utakuwa ni mgumu na itawaletea shida kubwa sana Wazanzibar. Kwa nini nasema hivyo? Kwa sababu hapa suala hili la mapato pia linakwenda kwenye mtambuka wa Wizara ya Biashara. Mikakati ya biashara ambayo ndiyo inapelekea mapato kwa pande zote mbili huwa ni suala la Wizara ya Biashara ambapo sasa Wizara ya Fedha kwa kutumia *TRA* wanakwenda kukusanya kodi.

Mheshimiwa Spika, sasa hapa inavyoonekana ni kwamba kwa upande wa Zanzibar, sera za Zanzibar za biashara zinakuwa zipo tofauti, lakini hata hivyo wananchi wake asilimia kubwa sana wanakipato cha chini ukilinganisha uchumi wa Zanzibar na uchumi wa Tanzania Bara ni mbingu na ardhi, vitu hivi si sawa kabisa kwenda kuweka kodi sawasawa ni sawa na kuwasema Wazanzibar wawe katika hali duni zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka lifanyiwe uchunguzi suala hili kwamba hali ya maisha ya watu wa Zanzibar hasa wafanyabiashara ni ile kwamba hawana jinsi ya kufanya, lakini kwa kweli biashara wanafanya kwa kujilazimisha; mitaji hawana na asilimia kubwa ya wananchi wa Zanzibar wanategemea wale wafanyabiashara kidogo kuwasaidia ili kuendesha maisha yao. Kama si hivyo ningesema asilimia 80 ya Wazanzibar tungeingizwa kwenye mpango wa *TASAF* ili kusaidiwa kwenye kaya maskini. Sasa sheria hii naona ingefanyiwa mabadiliko viwango vikabakia kuwa tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa pili nakwenda kwenye Sura Na.438 kwamba Wizara ya Fedha ama *TRA* itatambua walipakodi waliosajaliwa Zanzibar sawa na

walipakodi waliosajiriwa Tanzania bara. Suala hili pia ni sawa na lile ambalo limepita kwa sababu hii *database* ya *TRA* katika mfumo wa kupata *TIN* Zanzibar ipo kivyake na bara ipo kivyake. Hii inasaidia sana kwa maana ya kwamba sasa unapokwenda kuweka sasa ya aina moja maana yake ni nini? Itawafanya wafanyabiashara wale wa Zanzibar ambao kule kodi zake zinakuwa, kwa kweli kwanza uelewa wenyewe wa kutunza zile hesabu maana yake sisi kwa kweli kule kwetu biashara tunafanya kwa shida tu, hatufanyi kwa mitaji, hatufanyi kwa elimu, tunafanya kwa shida. Kwa maana hiyo, bado kwanza tunatakiwa sisi kama wafanyabiashara wa Zanzibar tubakie katika *database* yetu ile ile ya Zanzibar na *database* ya bara iwe vilevile na hakuna tatizo kwa sababu hata kwenye michango yetu ya bajeti hatukuchangia suala hili kwamba ni tatizo. Kwa maana hiyo mimi nashauri ibakie vilevile ili twende sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine pia katika sheria hii hii imesema kwamba *ZRB* itasaini makubaliano. Sasa haya makubaliano sasa mimi yananipa ukakasi kwasababu *ZRB* haina nafasi ya kufanya kazi Tanzania Bara, sasa makubaliano haya ndiyo yanatupa *direction* kwamba yanakwenda kuifanya *TRA* kule ifanye kazi zake lakini huku bara *ZRB* haina nafasi kabisa. Kwa maana hiyo bado nasema sura hii isiwe na mabadiliko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikiendelea kwenye kifungu cha 32; kuzuia kodi ya mapato ya mlipakodi wa pango la nyumba. Hili suala limekuwa likifanyika na sijui ni kwa nini hii sheria imekuja au lilikuwa linafanyika bila sheria lakini ninachoweza kusema ni kwamba mwenye majengo anafahamika na mfanyabiashara anafahamika kwa maana hiyo mfanyabiashara alitakiwa aachwe kuwa na kodi yake inayomuhusu na yule mwenye kodi ya majengo yaani mwenye nyumba basi naye afuatwe kwa namna Serikali itakavyojua kuliko kumwongezea mzigo mfanyabiashara kwenda kulipa kule na mara nyingi wale wenye nyumba

huwa hawataki kulipa ile *capital gain tax* ama ile kodi ya zuio. Kwa maana hiyo, nashauri kwamba bado kila mmoja aachiwe majukumu yake ya kulipa kodi.

Mheshimiwa Spika, pia nikija kwenye rufaa za kikodi kifungu cha 22 kimeelezea hivyo, kifungu hiki ni kifungu kandamizi, nakiita kifungu kandamizi kwa sababu hapa wanataka watoza kodi kusiwe na msuluhishi, maana yake mtoza kodi na mlipakodi wao kwa wao wamalizane. Sasa hakiwezekani kitu kama hiki, kwa maana ya kwamba huyu mlipa kodi kukiwa na *fault* yoyote hawezi kwenda popote kwenye chombo cha kisheria atamalizana na yule ambaye amemkosea. Sasa inakuwaje kwamba yule ambaye umemkosea, yeye ndiyo mkae pamoja na kusuluhisha hili haliwezekani, bado sheria hii nayo itakuwa haiwezekani kwa sababu bado sheria hata katiba inaruhusu chombo cha mwisho cha kutoa maamuzi ni mahakama, kwa maana hiyo bado iruhusu *TRA* kama kutakuwa na tatizo, basi mfanyabiashara anaweza kwenda mbele kutafuta haki yake.

Mheshimiwa Spika, mwisho nikimalizia ni katika Sura ya 394 kuhusu suala la Bima. Sura hii imeelezea kwamba kutoza Bima ya lazima kwa sehemu ya biashara, vivuko na mizigo inayotoka nje…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Spika, samahani, naomba nimalizie hii *point*.

Mheshimiwa Spika, ni kwamba mizigo inayotoka nje, tayari kule inakotoka ina *insurance*. Maana yake hata kodi zenu mnavyozifanya ni *Cost Insurance and Freight (CIF)*. Sasa kwa nini leo unakuja kusema ikatiwe *insurance* hapa ya lazima? Ina maana itakuwa ni *double insurance,* ni kumwongezea mzigo mfanyabiashara. Nadhani suala hili pia

halifai kwa sababu mzigo tayari umeshakuwa na *insurance*, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Serikali kwa usikivu wake wa kupokea na kufanyia kazi maoni yetu Wabunge na kisha kufanyia marekebisho baadhi ya maeneo yaliyoletwa kwenye hotuba ya Waziri wa Fedha na Mipango kwenye hotuba ya Bajeti Kuu ya Serikali kwa mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano; kuondoa 3.5% kama kodi ya magari makubwa na mabasi ya abiria na kutokuondoa 5% kwenye 10% ya fedha za mikopo kwa ajili makundi maalum kwenye mapato ya ndani ya halmashauri.

Mheshimiwa Spika, naendelea kuishauri Serikali kuwekeza ipasavyo kwenye sekta za uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

Mheshimiwa Hamad Chande, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, na Mtoa hoja ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimia Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami nichangie. Awali ya yote, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu *Rahim* ambaye ametujaalia rasilimali ya uhai hadi sasa, ambayo ndiyo thamani ya ubinadamu. Maana yake ikiondoka rasilimali ya uhai, basi thamani ya ubinadamu nayo imeondoka. Ushahidi wa hilo ni kwamba mtu huyo huchukuliwa na kupelekwa mbali kabisa na siyo katika makazi ya wanadamu wa kawaida.

Mheshimia Spika, kipekee naomba nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kiasi kikubwa anavyosikiliza kilio na machozi ya wananchi wake ambao ni watoto wake. Ushahidi wa hili nilisema juzi hapo kwamba mama ana upeo mkubwa sana wa kutafsiri chozi la watoto wake kwa vitendo. Nadhani Wabunge wenzangu wote ni mashahidi juu ya hilo. *(Makofi)*

Mheshimia Spika, kipekee naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwako kwa kiasi unavyoendesha vizuri na kwa ufanisi majadiliano ya Muswada huu na mengine ambayo yalipita.

Mheshimia Spika, napenda pia kumshukuru Waziri wetu wa Fedha na Mipango, kwa kiasi kikubwa anavyotoa maelekezo kwangu na kufanya kazi kwa ufanisi kwa pamoja. Mashirikiano yake nimeyakubali sana. *(Makofi)*

Mheshimia Spika, vile vile nawashukuru sana Kamati yako ya Bajeti, iko vizuri na inafanya kazi kwa ufanisi wakati wote. Saa 24 wako tayari kushirikiana nasi, wakiongozwa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mheshimiwa Sillo na Makamu wake Mheshimiwa Kigua, na Wajumbe wenzangu wote. Pia nawashukuru Wabunge wenzangu, tangu jana tulipoanza mjadala huu, mijadala yao ni ya kujenga tu. Kwa hiyo, niwahakikishie kwamba ushauri wao, mawazo yao, mapendekezo yao, Serikali imeyachukua na itayafanyia kazi kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimia Spika, nitazungumza tu kwa ujumla hoja chache. Hoja ya kwanza Waheshimiwa Wabunge wametoa hoja ama wamependekeza Serikali iendelee kutoa elimu juu ya umuhimu wa Bima ikiwa ni pamoja na kuanza kukata Bima kwenye mali zake kama vile magari. Ushauri huu umechukuliwa na tumeuzingatia na tutaufanyia kazi na tutatoa elimu kwa taasisi zote za Serikali, magari yao yote yawe na Bima pamoja wao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili ambayo imetolewa ni kwamba Serikali ifanye tathmini ya kina ya upungufu na mafanikio yaliyopatikana kutokana na utolewaji wa mikopo husika. Aidha, upungufu utakaobainika ufanyiwe marekebisho. Serikali imelichukua na itafanya tathmini ya kina sana hatua kwa hatua. Tunaelekeza Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani kufanyia kazi suala hili, tathmini hiyo na ripoti yake ipatikane haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimia Spika, kwa hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, sasa nimuite Mtoa hoja, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu, aje ahitimishe hoja yake.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimia Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuhitimisha hoja hii. Awali ya yote, namshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa mwongozo wake ambao ametupatia kuanzia kwenye mjadala wa Bajeti na kwenye mjadala huu wa kutunga sheria, ambapo ametupa fursa ya kuweza kuyasikiliza maoni ya Wabunge na kuyafanyia kazi. Narejea kauli yake, alisema, mtakapopokea mawazo haya, pamoja na kwamba mmeenda na mapendekezo yenu na mitizamo yenu, lakini lazima mwasilikize wawakilishi wa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimia Spika, sisi tuliokulia vijijini, tuliolima na majembe yale ya kukokotwa na ng'ombe, *speed* ya wale ng'ombe wa nyuma, huwa inafuata *speed* ya ng'ombe wa mbele. Ninyi ndio mnaweza mkaona hicho kimesaidia sana Wizara ya Fedha kuwa *flexible*, kuweza kusikiliza maoni ya wawakilishi wa wananchi ambao kwa kweli nikiri kwamba mmewawakilisha vyema sana wananchi wa Majimbo yenu na wananchi wa maeneo yaliyowachagua. *(Makofi)*

Mheshimia Spika, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Wajumbe wote wa Kamati ya Bajeti ya Bunge, pamoja na Makamu Mwenyekiti na Mwenyekiti, mtani wangu Ndugu Daniel Sillo kwa ushauri wao walioutoa wakati wa majadiliano ya Muswada ambao umesaidia kwa kiasi kikubwa sana katika kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kutambua michango ya Wabunge waliyoitoa hapa Bungeni, na niwaambie, kama ambavyo tulisema, kwa kiwango kikubwa tumeweza kutekeleza, kuyajumuisha maoni kama ambavyo mmetoa. Kamati ilipendekeza Serikali ianzishe tozo ya *parking fee*, *carbon emission fee* pamoja na *tollgates* kwa malori; Serikali imepokea mapendekezo hayo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *carbon emission,* kwa upande wa Tanzania, mtakumbuka zamani tuliwahi kuwa na utaratibu huo, lakini kwa ajili ya kupunguza usumbufu, tulijumuisha kwenye tozo nyingine ambazo zinatozwa, kama tulivyofanya kwa upande wa *road license*, badala ya kutoza *road license* kama Kifungu kinachojitegemea, nakumbuka tulijumuisha kwenye mafuta ili kupunguza tu usumbufu. Kwa hiyo, hata kwenye *carbonate emission* tulishafanya hivyo tukaweka kwenye tozo nyingine ili kuondoa utozaji wa mara mbili.

Mheshimia Spika, kwenye upande wa *tollgates* ilikuwepo na yenyewe kwenye upande wa barabara kuu hizi, lakini na yenyewe tuliiondoa kwa sababu ya kuwa na vizuizi vingi sana njiani. Mtakumbuka kuna wakati ilikuwa inatokea gari inaweza ikatoka kwenye mpaka mmoja, mpaka ikakize katikati ya nchi ya Tanzania, unakuta ilishasimama mara nyingi kwa idadi ya Wilaya mathalani. Jambo la aina hii lilikuwa linafanya muda uwe mrefu sana wa magari kupita ndani ya nchi kwenda maeneo mengine na ilikuwa inasababisha usumbufu wa wasafirishaji na vikwazo visivyo vya kikodi, vya kibiashara. Kwa maana hiyo, na yenyewe

tuliitengenezea utaratibu wake ambayo ipo kwenye sheria ile ambayo tulikuwa tunajadili inayohusisha magari ya kigeni yanayopita. Kwa hiyo, yenyewe ilishajumuishwa mle kwenye ulipiaji wa magari ya kigeni.

Mheshimia Spika, zile tozo tulizoziweka, nakumbuka na hiyo ilikuwemo kwenye uchangiaji, siyo tozo mpya. Tulichofanya kwenye Bunge hili la sasa, tumeshusha ile tozo tuliyokuwa tunatoza sisi kama nchi, tumeiwianisha na zile tozo zinazotozwa kwa upande wa *COMESA*, kwa upande wa *EAC*, ambapo sisi tulikuwa tunatumia *SADC* ambayo ilikuwa juu kuliko hizi. Tumerudisha ili iweze kuwiana na nchi nyingine. Kwa hiyo, hakuna athari ambayo itatufanya sisi tusiwe washindani tukilinganisha na nchi nyingine. Tumeishusha ili tuweze kulingana na wenzetu wa Kenya, Uganda na nchi nyingine ambazo ziko *COMESA* zinazotumia kiwango hicho ambacho mwanzoni sisi tulikuwa tunatumia kiwango kikubwa kuliko cha nchi wanachama tulionao kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimia Spika, Mheshimiwa Kandege, aliongelea kuhusu Serikali iwekeze kwenye matumizi ya mifumo. Ushauri wake ni mzuri tumeupokea. Mheshimiwa Halima Mdee, aliongelea kuhusu kuzingatia taratibu za urejeshwaji wa mikopo; ushauri huo ni mzuri, tumeuzingatia, tutateta na wenzetu wa TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Neema Lugangira, pamoja na Mheshimiwa Joseph Kakunda, waliongelea mapendekezo ya Serikali kuangalia utaratibu wa *pump* za maji. Tumepokea ushauri huo. Mheshimiwa Japhet Hasunga, aliongelea jambo lake lile na nilishalifafanua kwenye maeneo yale ambayo yalikuwa bado yanahitaji ufafanuzi tumeielezea kwa kirefu kwenye badiliko letu kwamba, siyo kodi mpya isipokuwa tumetengeneza utaratibu wa kuweza kutofautisha na kuweka ufanisi zaidi. Ila siyo kodi mpya, ni kodi ambayo ilikuwepo. Mheshimiwa Shamsi Vuai, ameelezea kuhusu

upande wa masuala ya utalii, Serikali imepokea ushauri wake.

Mheshimia Spika, *Engineer* Mwanaisha aliongelea kuhusu suala la ukusanyaji wa tozo. Ni kweli, ushauri alioutoa ni wa msingi kabisa. Naomba niweke hilo pendekezo ambavyo inatakiwa kusomeka, nadhani tulikuwa tumeweka kwenye maelezo yetu. Wakati nasoma hotuba, ni kweli nilitaja hivi vitu vya *tollgates.* Tunatarajia kujenga *expressway* kutoka Kibaha kuja mpaka Morogoro. Tulikuwa tunaangalia pia *expressway* ya upande wa kwenda mpakani kule Mbeya kwenda Tunduma. Pia kwenye Hotuba ya Bajeti tuliongelea upande wa *Tanzanite* ambapo tathmini bado inafanywa na Wizara ya Kisekta kuona *feasibility* kama jambo hilo litakuwa *feasible* kwa kiwango gani?

Mheshimia Spika, napendekeza kurekebisha Sheria ya *The Road and Fuel Tall Act* ya Cap. No. 220 katika Kifungu cha 7(2) kwa kuongeza Kifungu kidogo cha 7(2)(d) ili viweze kusomeka kama ifuatavyo: Ile (d) isomeke: *"The owner or the driver of the vehicle passing through the specific public road as may be specified by the Minister responsible."* Kifungu hiki kitampa Waziri wa Fedha kutangaza barabara ama madaraja yanayopaswa kulipiwa *road tall*. Aidha, napendekeza kurekebisha Kifungu cha 7 cha sheria hii na kuongeza kifungu kipya kidogo cha 7 kisomeke kama ifuatavyo: *"the rate of the road tall and the public road in the respect of which such a tall shall be payable may be prescribed by the order in the gazette."* Kifungu hiki kitamwezesha Waziri wa Kisekta kubainisha kupitia hati itakayotolewa na Waziri wa Fedha.

Mheshimia Spika, Mheshimiwa Kunambi, ameongelea jambo linalohusisha misamaha ya miradi ya maendeleo. Tumepokea ushauri, tutaangalia kiutawala hili jambo linafanyikaje? Utaratibu Serikali iliokuwa inatumia, zamani miradi hiyo hati zake zilikuwa zinatolewa na Waziri. Kwa ajili ya

kuweka ufanisi, tukaisogeza kwa Kamishna wa Mapato ili awasiliane na Mameneja wake wa Mikoa ili waweze kusaidiana katika kuharakisha jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kiutawala tutaliangalia hili ili kuweza kuweka ufanisi mkubwa zaidi ili miradi isichelewe kwa sababu ya jambo hilo, huku tukidhibiti. Tuliweka chini ya Mamlaka ya Kamishna Mkuu kwa ajili ya udhibiti ili kuweza kuhakikisha kwamba misamaha hiyo haichepushwi. Kwa sababu pakiwa na hatua kidogo za kiudhibiti miradi hiyo inaweza ikatumika kupitisha misamaha ambayo haiko kwenye miradi ile ambayo imekusudiwa.

Mheshimia Spika, kwa upande wa jambo la Mheshimiwa Mwambe, ameelezea kuwa fedha zile zielekezwe kwenye korosho. Jambo hili tumelizingatia sana na Wizara ya Kilimo iko makini kwenye jambo hili. Kwa sababu kuna taratibu ambazo zinaendelea kufanyika ambapo Wizara ya Kisekta inafanya mageuzi katika sekta mbalimbali ikiwemo hiyo ya upande wa zao la korosho, tuliona tupeleke kwenye Wizara ili usimamizi uweze kufanyika kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kwamba kuna wakati fedha zilikuwa zinaenda kwenye Bodi, kuna maeneo haikufanya vizuri sana. Ndizo sababu za kimatumizi zilizosababisha fedha hizo zikaamuliwa ziende kwenye Mfuko Mkuu. Kwa hiyo, bado tunaamini tuiachie Wizara ili iweze kuratibu na nia ni hiyo hiyo ambayo Mheshimiwa Mbunge amesema, ndicho ambacho na Wizara wanalenga kukifanya.

Mheshimiwa Spika, kwenye vipengele vile vingine alivyokuwa anapendekeza kutengeneza mgao zaidi, tulikuwa tunaomba Mheshimiwa Mbunge aridhie kwamba tuna masuala ya kibajeti ambayo yanatulazimisha kuendelea kutunisha Mfuko Mkuu. Kwa mwaka mmoja kupandisha bajeti kutoka Shilingi bilioni 200 kwenda zaidi ya Shilingi bilioni 900,

na utakumbuka wakati ule nasema hapa, nilisema bado tunaendelea pia na mashauriano, ambapo kwenye Wizara ile ya Kilimo kuna *component* nyingine ambayo itahusisha *private sector*, kwa maana ya utoaji wa *LC* pamoja na mengine. Tunaendelea kuongea na benki za nje, huenda bajeti hii ya kilimo ikazidi shilingi trilioni moja kwa zaidi ya shilingi bilioni 100 nyingine, kwenye ile sehemu ambayo tutahusisha sekta binafsi na yenyewe itakapoingia kwenye eneo hilo la kilimo. *(Makofi)*

Mheshimia Spika, kwa hiyo, tunapopandisha bajeti hivi, kuna fedha tunazitoa katika maeneo mengine. Kwa mfano, fedha za ruzuku ya mbolea zitatoka kwenye Bajeti Kuu, lakini pia na fidia za maeneo mengine ambayo tumesamehe. Kwa hiyo, tuliomba hata Wizara ya Kisekta ilikuwa na kiu hiyo hiyo ya kuona tunapeleka fedha zaidi, lakini tuliwaomba waone kwamba tuna majukumu mengine ya kuweza kufidia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, hapa tutahitaji kuweka fidia kwenye kupoza gharama za maisha kwenye mafuta ya magari au mafuta haya ya nishati. Pia tumeongeza fedha ambazo zinatakiwa ziende kwenye elimu bure pamoja na maeneo mengine yale ambayo yameongeza fedha. Haya yote yatahitaji yafidiwe kwenye Mfuko Mkuu. Utaona kwamba pengo lile ambalo linatakiwa kuzibwa linahitaji tuokote fedha kutoka katika maeneo mengine na hicho ndicho ambacho tumekitumia.

Mheshimia Spika, Mheshimiwa Mpina ameongelea kuhusu miradi hii ya wawekezaji mashuhuri kwamba kuipeleka kwenye Baraza la Mawaziri itasababisha Serikali yote iingie. Tukiwaza katika sura ya kimakosa kwamba hivi vitu vinaweza vikapitishwa kimakosa, tunaweza tukapata picha hiyo anayoisema Mheshimiwa Mpina. Ila tukiwaza katika sura ya kuweka ufanisi, ukipeleka kwenye Baraza la Mawaziri ndipo ambapo utapata ufanisi mkubwa zaidi. Kwa sababu ili

jambo liende kwenye Baraza la Mawaziri kwanza lazima litakuwa limetoka kwenye kikao hicho cha *NISC* ambacho Mwenyekiti wake ni Waziri Mkuu, lakini likienda kwenye Baraza la Mawaziri kabla halijaenda kwenye Baraza la Mawaziri, lazima lipite kwenye kikao cha Makatibu Wakuu wote wa Serikali ambako Mwenyekiti wake ni Katibu Mkuu Kiongozi.

Mheshimiwa Spika, vile vile kabla halijaenda kwenye Baraza la Mawaziri ambapo Mwenyekiti wake ni Rais, lazima vyombo vyake vyote vinavyomsaidia Rais viwe vimeshafanyia uchambuzi. Sisi tulidhani likifanyika hivyo, tunakuwa tumejihakikishia zaidi ufanisi katika Taifa kuliko kupeleka jambo hilo kwa Waziri peke yake ambaye hana vyombo kwa kiwango kile cha kuweza kumfanyia uchambuzi wa kiwango hicho. *(Makofi)*

Mheshimia Spika, Mheshimiwa Mpina anasema ikienda kwenye Baraza Waziri atapata mwamvuli, kwa hiyo, atakuwa amepata kinga, hiyo tutakuwa tunawaza katika namna ya kuacha jambo litokee, tupate kwanza hasara, halafu tuhangaike na kumwajibisha Waziri. Tukipeleka kwenye vyombo vya nchi nzima ambavyo vitafanyia tathmini, tutakuwa tumehangaika na kuzuia matatizo yasitokee, kuliko kusubiri matatizo yatokee ndiyo tuanze kuhangaika na matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naamini kwamba mapendekezo haya Serikali iliyoleta yanalenga zaidi kulinda rasilimali za Watanzania, na hiyo ndiyo dira ya Mheshimiwa Rais. Anatamani rasilimali za Watanzania zilindwe. Tusihangaike na makovu, tusihangaike na hasara, tulinde hasara zisitokee, tulinde maovu yasitokee, tuhakikishe kwamba rasilimali za wananchi zinatumika katika matumizi yaliyokusudiwa.

Mheshimia Spika, nimalizie la mwisho. Mheshimiwa Mohamed Issa ameongelea jambo la *ZRB* pamoja na *TRA*. Mheshimiwa Mbunge ametoa hoja nzuri, isipokuwa

namwomba aipitie kwa undani zaidi. Hicho alichokuwa anakisema, *actually,* mapendekezo haya yanalenga kuwasaidia wananchi wa Zanzibar. Kwa sababu walikuwa wanapata usumbufu. Hii haiendi kuongeza wala kupunguza. Ilikuwa mlipa kodi huyo huyo inabidi waje watu wa aina mbili ama tatu zaidi wanaotoka kwenye nchi hiyo hiyo. Tulichofanya, ametolea mfano, akasema, mbona *mainland ZRB* haiji? Hicho ndicho tunachofanya, kwamba hapa ingekuwa *TRA* inakusanya, halafu makusanyo ambayo ni ya upande wa Zanzibar kwamba *ZRB* ije kukusanya huku, tungekuwa tunatengeneza usumbufu.

Mheshimiwa Spika, kuna kodi ambazo zinahusu Zanzibar, lakini *ZRB* huwa haiji kukusanya, *TRA* ndiyo huwa inakusanya ina-*remit* kwa upande wa Zanzibar. Kwa mfano, mawasiliano; hata miamala inayotumwa upande mwingine, mkusanyaji anakuwa mmoja, mgawanyo unafanyika kufuatana na sheria inasemaje. Hata huko Zanzibar tumesema kwa sababu mifumo ilishakuja kurahisisha kazi si jambo la busara, nikope msemo wa Mheshimiwa Halima; "si busara mifumo, imeshakuja ya kurahisisha utaratibu huo sisi tuendelee kutuma watu kwenda kuwasumbua watu mara mbili mbili."

Mheshimiwa Spika, tukasema yule aliyopo pale akusanye, halafu namba zinasema kipi ni kipi, tunakuwa tumeshawapunguzia usumbufu wa kufuatwa na watu mara nyingi nyingi. Kwa hiyo, ndicho tulichokifanya, hakiendi kuwaongezea mzigo Wazanzibar, *actually* kinakwenda kuwapunguzia usumbufu na jambo hili tumekaa vikao vingi vya Wizara ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Wizara ya Fedha ya Zanzibar tukiishirikisha na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar ili vitu vyote vinavyohusisha pia kisheria viweze kutengemaa. Lakini lengo ni kuongeza ufanisi katika ukusanyaji.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini si mwisho kwa umuhimu, Waheshimiwa Wabunge tunakwenda majimboni, tunakwenda kwa wapiga kura wetu katika kipindi ambacho nchi iko kwenye zoezi la sensa. Rai yangu kwenu, nawaombeni twende tukatoe elimu kwenye masuala ya sensa, tuwahamasishe wananchi wajitokeze kwenye masuala ya sensa; tuwaelimishe wananchi sensa ni kwa ajili ya maendeleo yao; sensa ni kwa ajili ya mipango ya nchi yetu; sensa ni kwa ajili ya maisha yao wao wenyewe. Wasiendelee kupotoshwa na baadhi ya watu ambao bado wana mila zile potofu zinazopotosha masuala haya ya sensa.

Mheshimiwa Spika, misemo mingine ile ilikuwa misemo tu ambayo ilikuwa inanogesha, tumeambiwa maneno mengi sana, zamani tulikuwa tunaambiwa usile mayai utapata kipara, kumbe walikuwa wanataka tu wazazi wetu watakapokwenda kazini wasikute mayai yote pale nyumbani yameshafanyiwa kazi. Kwa hiyo, hata hii habari kwamba usihesabiwe sijui ukihesabiwa itakuwaje, hizo zilikuwa *story* za mijadala tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sensa ni kwa ajili ya maendeleo, duniani kote masuala ya sensa yanafanyika na Waheshimiwa Wabunge niwahakikishie kama kuna vipeperushi vinatakiwa ili mfanye semina vizuri; nitawaelekeza wataalam wetu wawapatie vipeperushi, kama mtatakiwa mpate tai kama ya Mheshimiwa Naibu Waziri pale na vilemba vya sensa kwa ajili ya hamasa, hivyo na vyenyewe tutatoa na maandiko yote ambayo yameshatolewa ambayo yanahusiana na sensa ili mkatoa elimu tutatengeneza utaratibu ili muweze kupata na hatimaye mkatoe elimu na wananchi wote washiriki kikamilifu zoezi hilo la sensa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya naomba sasa kutoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana.

Niwatangaze wageni ambao wameingia baada ya tangazo lile lingine la wageni kabla hatujaendelea na ratiba yetu.

Wapo wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge ambao wameingia baada ya tangazo la wageni, wasimame wote kwa pamoja wageni wa Waheshimiwa Wabunge, kKaribuni sana, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunao pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, wanafunzi 82 na walimu 10 kutoka Shule ya Sekondari ya Wasichana ya *Queen of Family* kutoka Kahama, Mkoani Shinyanga, karibuni sana, sana sana Bungeni. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:** Kamati ya Bunge Zima.

**SPIKA:** Kamati ya Bunge zima.

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2022**
***(The Finance Bill, 2022)***

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2
Kifungu cha 3

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 4

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 5
Kifungu cha 6

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 7

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 8
Kifungu cha 9
Kifungu cha 10
Kifungu cha 11
Kifungu cha 12

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Haya sasa tutawahoji kwa namba zinazoonekana hapa halafu mwishoni tutabadilisha hizi namba za vifungu.

Kifungu cha Kipya 13

*(Kifungu Kipya kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima)*

Kifungu cha 14

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecil Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeleta kwako makusudio ya kutaka kuona Kifungu hicho kinafanyiwa marekebisho ambacho kwa wale wanaofuatilia kipo ukurasa wa saba.

Mheshimiwa Mwneyekiti, sheria hii *Amendment of the Cashewnut Industrial Act, Cap.* 203; labda niisome ili niweze kuijenga hoja yangu kuanzia hapo. Kwenye kipengele cha 13 kinasema *this part shall be read as one with the Cashewnut Industrial Act, hereafter referred to as the "principal Act*."

Kipengele cha 14; *"The principal Act is amended in section 17A by deleting subsection (2) and substituting for the following;* kipengele cha (2); *"The total amount of export levy collected under subsection (1) shall be distributed in the following manner*."

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa (a) nina marekebisho madogo tu kwenye *schedule* yangu niliyoileta kwako nimetaka maneno yafutayo yaongezwe; kadiri ya Mheshimiwa Waziri na Serikali wameleta wanasema *50 percent shall be remitted to the Ministry responsible for Agriculture....*

**MWENYEKITI:** Sasa ili nikutunzie muda wako soma marekebisho yako, ya Serikali tunayo.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, marekebisho yangu nataka yaongezwe kama ifuatavyo; kwenye mstari wa mwisho isomeke *subsidy on cashewnuts;* kwa sababu hii pesa iwe *ringfenced on cashewnuts* na kipengele kinachofuata (b) iwe *specific* ioneshe mara mbili, asilimia 15 iende kwenye *Agriculture Development Fund* na asilimia 35 iwe *remitted* kwenye *Consolidated Fund,* ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Kilimo.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni *acknowledge* mawazo mazuri ya Mheshimiwa Mbunge, lakini nilitaka niombe kwamba kwenye *amendment* yake *item (a)* anayosema kwamba 50 *percent shall be remitted to the Ministry responsible for Agricultural inputs subsidy as a Government* tunakubali maoni ya kwamba hii *subsidy* iwe *specifically for cashewnut*. *(Makofi)*

Kwa hiyo, *what you can say* tutasema kwamba *50 percent shall be remitted to the Ministry responsible for Agriculture, for agricultural input subsidy on cashewnut and Agriculture Development Fund;* ili kui-*ringfence* ionekane kwamba inakwenda *specifically* kwenye kutoa *subsidy* ya korosho.

**MWENYEKITI:** Si ndicho alichoandika?

**WAZIRI WA KILIMO:** Alicho-*propose*.

**MWENYEKITI:** Alichoandika yeye kasema hivi, isomeke *50 percent shall be remitted to the Ministry responsible for Agriculture, for Agricultural inputs subsidy on cashewnuts.*

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *yes, I agree, we agree.*

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, hakuna unachobadilisha?

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hakuna ninachobadilisha, tunaendelea naye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *component* ya pili ambayo ana *propose* kwamba *50 percent shall be remitted to the consolidated fund, proposal* ya Mheshimiwa Mwambe ni kwamba anataka kwenda kwenye *Consolidate Fund* iende *35 percent* na *15 percent* iende kwenye *Agricultural Development Fund* ukisoma hiyo *proposal* aliyoleta.

Kwa hiyo, mimi nilitaka nimuombe tuiache hii *50 percent* ibaki kama ilivyo kwenda kwenye *Consolidated Fund* na *reason* ni moja, kwa mwaka huu wa fedha *funding* kwenda ku-*support Agricultural Development Fund*, Serikali imetoa *150 billion shillings to support the ADF* kwa ajili ya ruzuku ya mbolea, lakini vilevile kwa mwaka huu tuna *negotiation* na *African Development Bank* ambapo tutapata *addition* ya *40 million dollars* kwa ajili ya kuingia kwenye *ADF*.

Kwa hiyo, ningeomba kwamba kwa mambo yalivyo, ningemuomba kwamba *component number two* tuiaiche kama ilivyo, tusibadilishe *50 percent* ibaki *Consolidated Fund*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa Waheshimiwa Wabunge kabla sijarejea kwa Mheshimiwa Mwambe, kwa utaratibu wetu wa utungaji sheria uko hivi, ukishaletwa muswada, yanaletwa marekebisho, halafu yanaletwa marekebisho juu ya marekebisho. Sasa hayo marekebisho ya Mheshimiwa Waziri mimi sina hapa mezani. Kwa hiyo, maana yake kama tunaafikiana na marekebisho ya Mheshimiwa Mwambe ndiyo

niliyo nayo hapa mezani, yaani utungaji wa sheria ule ambao ukifika ngazi hii tunaweza kufanya hayo marekebisho, ni yale marekebisho ambayo yaani siyo marekebisho kwa neno la Kiswahili siyo marekebisho ya msingi. Ni yale marekebisho ya kwamba sasa hii sheria itakuwa haijakaa sawasawa, ukioanisha vifungu na mambo kama hayo. Lakini haya sasa yanayoletwa juu ya marekebisho mengine siko nayo haya mezani, kwa hiyo tunakuwa tumefungwa kikanuni.

Kwa hiyo, kama tunakubaliana Serikali, kama mnakubaliana kimsingi na marekebisho ya Mheshimiwa Mwambe ndiyo haya hapa niko nayo.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tulichokiweka, tumeweka na ndiyo nilichosema pale wakati tunajibu, tumeweka ile *50 percent* inakwenda kwa ajili ya zao la korosho inapitia tu kwenye Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwneyekiti, lakini la pili lile alilolisema Mheshimiwa Mwambe sisi hatujarekebisha; kwa maana hiyo sisi tunakubaliana tu na pendekezo moja; lile pendekezo la pili analolileta hatukubaliani nalo kwa sababu tuna fedha zingine ambazo zita-*serve the same purpose*. Kwa maana hiyo, lile pendekezo la Serikali, tulivyoleta sisi kwenye pendekezo la Serikali linakwenda sambamba litakwenda moja kwa moja kwenye *50 percent* ndiyo tuliyoiweka inakwenda kwenye korosho.

**MWENYEKITI:** Sasa hapa jamani kifungu cha 14 cha Serikali kina asilimia 50 inakwenda kwenye *Agricultural Development Fund* na asilimia 50 inakwenda *Consolidated Fund*. Marekebisho ya Mheshimiwa Mwambe ambayo yanakuja baada ya Serikali yaani haya ya Mheshimiwa Mwambe yakija yamekuja kwenye kifungu cha Serikali, yanasema 50 iende kwenye *Agricultural input subsidy on cashewnuts; 15 percent Agricultural Development Fund; 35*

*percent* iende *Consolidated Fund;* haya ndiyo marekebisho yaliyopo kuhusu kifungu cha Serikali; hakuna marekebisho mengine yaliyokuja kwamba sawa tunakubali *cashewnuts* maana ndivyo kifungu kitatakiwa kusoma, kitatakiwa kusoma marekebisho ya Mheshimiwa Mwambe kwa mapendekezo yenu, yasome Mheshimiwa Mwambe tuchukua (a) halafu (b) tuchukue Serikali. Si ndiyo mapendekezo yenu?

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa hiyo *wording* ilitakiwa ifanyiwe *schedule* basi sisi tuliombe Bunge lako tukufu kwamba hatuna sehemu nyingine ya kupeleka hiyo *50 percent* ni kwenye korosho huko huko, inakwenda kwenye korosho; Mheshimiwa Mbunge aiamini Serikali *50 percent* inakwenda kwenye korosho, haiendi kwingine. Halafu *50 percent* ile iende Mfuko Mkuu itakuwa ime-*serve the same purpose*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ili tuwe tumeelewana vizuri, kwa sababu hofu ya Mheshimiwa Mwambe mpaka ameleta haya marekebisho ni ile anataka asilimia 50 isiende kwenye Mfuko wa Jumla iende wapi kwenye kkorosho na Serikali inasema hivi, yenyewe haijaweka neno korosho hapa, lakini kwa namna ilivyomuelewa Mheshimiwa Mwambe na Wabunge wengine walivyochangia hii asilimia 50 bora iende wapi kwenye korosho.

Sasa kwa utaratibu wetu wa kikanuni, hoja ya Mheshimiwa Mwambe iko hapa na hoja ya Serikali kama ilivyo bado iko hapa mbele, nadhani tuelewane hapo vizuri. Hoja ya Mheshimiwa Mwambe ipo hapa mbele ipo na hoja ya Serikali ipo mbele. Sasa kwa utaratibu ulivyo yaani lazima tuletewe yale mabadiliko, kwa sababu hatuna Mheshimiwa Mwambe atapewa fursa ya kuhitimisha hoja yake. Kama yeye ameielewa Serikali atasema, kama hakuielewa kikanuni tutahoji marekebisho ya Mheshimiwa Mwambe.

Mheshimiwa Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Mimi nakubaliana na mapendekezo ya Serikali kwa sababu wamekubaliana na mimi kwenye kipengele (a) na kuliingiza pale neno korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka tu nitoe maelekezo kidogo kwamba hata huko nyuma bajeti zetu zimekuwa zikitegemea misaada, *grants* na vitu vingine kutoka maeneo mbalimbali. Tumeona kuna wakati bajeti haiendi vizuri kwa sababu wafadhili ama watu wengine hawajaleta fedha ya kuchangia kile walichokiahidi, inapokosekana ndiyo kuna kuwa kunashida. Sisi tumeamua kama Serikali, tumeona bajeti kubwa sana iliyokwenda Wizara ya Kilimo, sasa kama Serikali imeamua hivyo na sisi kama Wabunge tumeishauri kwamba tunataka tuone nchi yetu inapiga hatua kwenye masuala ya kilimo kwa maana ya kuongeza tija kwenye uzalishaji. Ndiyo maana tumeanzisha Mfuko wa *ADF,* lakini kuna ahadi za watu kuuchangia. Kwa nini Serikali isione haja tutakapokuja kwenye robo mwaka kubadilisha sheria zingine kama watakuwa wameshapokea hizo fedha zingine hii *15 percent* wakaiacha ikaendelea kama ambavyo walipanga mwanzoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, bado nasisitiza kwa hatua ya sasa Waheshimiwa Wabunge mniunge mkono asilimia 15 itamkwe wazi inakwenda *Agricultural Development Fund* kwa sababu hatujapokea hizo fedha za wafadhili na 35 inayobakia iende kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Endapo sasa wafadhili wataleta zile fedha kwa ajili ya kuchangia maendeleo ya kilimo ya Tanzania ya wote ndipo hii *15 percent* tutaiondoa na kwenda kuimalizia tena kwenye *Consolidated Fund*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawa, Waheshimiwa Wabunge mmeshasikiliza mawazo ya pande zote mbili; Mheshimiwa Cecil Mwambe ameshikilia mawazo yake, kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge nitawahoji. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa *guidance* uliyotoa kwa sababu sisi tulielewa *amendment* ilikuwa ni (a) kwamba kaweka marekebisho kwenye *item (a)* anataka neno *cashewnut* liingie, *item (b)* ambayo ni *50 percent* anataka tui-*split,* kwa hiyo, kama kwa *guidance* uliyoitoa namna hii ningeomba na Wabunge waiamini Serikali, tuache kama mapendekezo yalivyo, tutakwenda kutengeneza kanuni ambazo zitamuonesha mgawanyo wa hii fedha na namna ambavyo itaweza kwenda kutumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mwaka huu bila ya uwepo wa sheria, bila ya uwepo wa mabadiliko ya sheria, tumeweza kuipatia sekta ya korosho fedha zilizokusanywa kwenye *export levy* na kwenda kutoa ruzuku. *(Makofi)*

Niwaombeni Waheshimiwa Wabunge muiamini Serikali na mtuamini, tutakwenda kutunga kanuni ambazo zitasema *50 percent* itakwenda kwenye korosho; kanuni hizo zitaweza kuisimamia. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge wakubaliane na *proposal* hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa Waheshimiwa Wabunge kikanuni Mheshimiwa Mwambe alikuwa ameshahitimisha hoja yake kwa hivyo nilipaswa kuwahoji. Sasa Mheshimiwa Waziri hapa kasimama nikampa nafasi amefungua tena hoja, Mheshimiwa Mwambe hitimisha hoja yako.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nikushukuru sana na nipokee maelezo aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri na tukiamini kwamba tunaipa imani kubwa sana Serikali yetu na ninaamini kwamba kanuni

zitaletwa hapa ili tuzipitie na kuona namna ya ku-*accommodate* asilimia 15 pamoja na hiyo asilimia 35. Kwa hiyo, nimuombe tu wakafanye hicho walichokiahidi ili iweze kupata manufaa kwa wakulima wa korosho na bodi yetu ya korosho. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa ngoja ngoja pamoja na makofi, Mheshimiwa Mwambe naona hapa mwishoni umechanganya mambo kidogo.

Kanuni wanazokwenda kutengeneza siyo kwa ajili ya kukubali wazo la asilimia 15, 35; kanuni watakayokwenda kuweka ni kwa kuongeza neno korosho. Uwe umeelewa vizuri hoja ya Serikali ili usije ukasema tulichokubaliana sicho, Hapana. Sasa hivi hakuna tena nafasi ya wewe kuzungumza, Serikali haijakubaliana nawe kuhusu kupeleka asilimia 15 huku na kupeleka asilimia 35 huku, hapana. Serikali ilichokubaliana nawe ni kwamba ile asilimia 50 iende kwenye korosho, ndiyo walichokubaliana nawe.

Sasa Mheshimiwa Waziri kwa maelezo uliyoyatoa hapo na Mheshimiwa Mwambe kwa namna alivyohitimisha hoja yake Waheshimiwa Wabunge hapo hakuna hoja maana yake hoja yake amefanya nini, ameiondoa kwa maelezo aliyotoa hapa mwisho. Isipokuwa sasa kwa upande wa Serikali, kwa sababu tupo kwenye ngazi ya kutunga sheria, kwa sasa hivi kwa sababu mwaka wa fedha wa hii sheria tunayoanza inaanza tarehe 1 Julai, 2022, Mheshimiwa Rais akiridhia na kwa sababu hii ipo kwenye sheria, kanuni hazitaweza kufanya hayo marekebisho, ila kwa ajili ya kuweka utaratibu mkaweke utaratibu wenu huko, kwa sababu kanuni baadaye zitakuja kwenye ile Kamati yetu ya Sheria Ndogo, halafu tutasema mlitengeneza kupitia kifungu gani.

Kwa hiyo, kwa kuwa kuna Bunge linalohusu utungaji wa sheria linakuja basi mtaleta marekebisho haya ili kuweka hizo

fedha ziwe kwa ajili ya korosho kama mlivyoahidi hapa Bungeni. Nadhani nitakuwa nimeeleweka. Marekebisho haya yatakuja kwa marekebisho ya sheria. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mwambe ameshaitoa hoja yake kwa hivyo hoja nitakayokuwa nawahoji ni ya kifungu hiki kama kilivyokuwa kimeletwa na Serikali.

Kifungu cha 14

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 15
Kifungu cha 16

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 17
Kifungu cha 18

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 19

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilifutwa)*

Kifungu cha 20

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 21
Kifungu cha 22

Kifungu cha 23
Kifungu cha 24
Kifungu cha 25
Kifungu cha 26

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 27

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 28
Kifungu cha 29
Kifungu cha 30
Kifungu cha 31
Kifungu cha 32
Kifungu cha 33

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 34
Kifungu cha 35
Kifungu cha 36

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 37

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 38

*(Kifungu kilichotajwa hapo kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 39

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 40

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 41
Kifungu cha 42
Kifungu cha 43
Kifungu cha 44
Kifungu cha 45
Kifungu cha 46
Kifungu cha 47
Kifungu cha 48

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 49
Kifungu cha 50
Kifungu cha 51

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 52
Kifungu cha 53
Kifungu cha 54

Kifungu cha 55
Kifungu cha 56

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 57

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 58

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 59

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 60

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilifutwa)*

Kifungu cha 61

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu Kipya cha 62

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 62

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kifungu cha 62 Serikali...

**MWENYEKITI:** Hebu ngoja, kifungu cha 62 kina marekebisha ya Serikali, naona hapo...

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

Kifungu cha 62

*(Kifungu kilichotajwa hapo juukilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Kifungu Kipya cha 63

*(Kifungu Kipya kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 63
Kifungu cha 64

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu Kipya cha 65

*(Kifungu Kipya kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 65

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 66
Kifungu cha 67

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 68

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 69

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 70
Kifungu cha 71

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 72

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge na Serikali, tunatunga sheria hapa, kifungu cha 72 kinaafikiwa?

Kifungu cha 72

Kifungu cha 73
Kifungu cha 74

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 75

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 76

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 77

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 78

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 79
Kifungu cha 80
Kifungu cha 81
Kifungu cha 82
Kifungu cha 83

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilifutwa)*

Kifungu cha 84
Kifungu cha 85

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 86

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 87

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 88

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 89
Kifungu cha 90
Kifungu cha 91

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 92

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 93
Kifungu cha 94
Kifungu cha 95

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 96

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 97
Kifungu cha 98

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 99
Kifungu cha 100

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilifutwa)*

Kifungu cha 101
Kifungu cha 102

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 103
Kifungu cha 104

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 105

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu Kipya cha 106

*(Kifungu Kipya kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu Kipya cha 107

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 107
Kifungu cha 108

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 109

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 110

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu Kipya cha 111

*(Kifungu kipya kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 111

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 112

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 113

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 114

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilifutwa)*

Kifungu cha 115
Kifungu cha 116
Kifungu cha 117
Kifungu cha 118
Kifungu cha 119
Kifungu cha 120

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 121
Kifungu cha 122

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilifutwa)*

Kifungu cha 123
Kifungu cha 124

Kifungu cha 125
Kifungu cha 126

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu Kipya cha 127

*(Kifungu Kipya kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 127
Kifungu cha 128

*(Vifungu vilivyotajwa hapo vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 129

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilifutwa)*

Kifungu cha 130
Kifungu cha 131
Kifungu cha 132

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 133

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 134

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 135

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya marekebisho hayo, sasa vifungu vyote vimepangwa upya kwa mtiririko unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Kabla Bunge halijarejea Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri wakati akihitimisha hoja yake hapa, ametaja marekebisho kadhaa hivi ya sheria ambayo hayamo kwenye haya marekebisho. Kwa hivyo, hayo marekebisho siyo sehemu ya hii sheria iliyopitishwa leo.

Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Mtoa hoja taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima limepitia Muswada wa Sheria ya Fedha, 2022 *(The Finance Bill, 2022)* kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba taarifa hiyo sasa ikubaliwe na Bunge Zima.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Kwa utaratibu wetu Waheshimiwa Wabunge nitawahoji. Wanaoafiki hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka, 2022 *(The Finance Bill, 2022)*.

Waheshimiwa Wabunge, wote wameafiki, haya ahsanteni sana. Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria kwa ajili ya kutunga Sheria itakayotoza au kubadilisha baadhi ya kodi, ushuru, tozo na ada mbalimbali, kufanya marekebisho kwenye Sheria Mbalimbali zinazohusu Ukusanyaji na Usimamizi wa Mapato ya Umma *(A Bill for an Act to Impose and Alter Certain Taxes, Duty's, Levy's, Fees and to Amend Certain Written Laws relating to the Collection and Management of Public Revenues)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

*(Muswada wa Sheria wa Serikali Ulipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada umeshasomwa kwa Mara ya Tatu na kwa utaratibu wetu wa kutunga Sheria Kikatiba tumeshamaliza kwa sehemu yetu kama Bunge na sasa tutampelekea Mheshimiwa Rais ili na yeye afanye kwa sehemu yake kwa mujibu wa Katiba yetu

Ibara ya 97(1). Kwa hiyo, Bunge tumehitimisha kazi ya kutunga Sheria ya Fedha ya mwaka, 2022.

Waheshimiwa Wabunge, nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri namna ambavyo mmetoa ushirikiano mkubwa sana kwa Kamati yetu ya Kudumu ya Bajeti, namna ambavyo mlikuwa na utayari wa kusikiliza maoni yao, tumeona nia hiyo mpaka dakika za mwisho mlikuwa tayari kabisa kuendelea kuleta mabadiliko kama hiyo nafasi ingeweza kutolewa. Ni jambo jema sana kwa Serikali kusikiliza mawazo ya Waheshimiwa Wabunge, siyo tu kama wawakilishi wa wananchi lakini kama watu ambao wanayo mawazo mengi yanayotoka kwa wananchi. Kwa hiyo, ni jambo jema sana kwa Wizara ya Fedha kufanya hivyo na mimi nawapongeza sana Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote ambao mnafanya kazi pamoja nao ni jambo zuri sana. *(Makofi)*

Pia niwapongeze sana Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, imefanya kazi kubwa sana kipindi hiki chote. Waheshimiwa Wabunge mpaka kufika leo hapa tukihitimisha safari yetu ya kupitisha bajeti na kupitisha sasa Sheria ambayo itaiongoza Serikali namna ya kwenda kukusanya hayo mapato ambayo wao walishatuletea makadirio wanakusudia kuzipata vipi hizo fedha, sasa Sheria imeshapita hapa. Kwa hiyo, Kamati yetu ya Bajeti imefanya kazi kubwa sana, tunawashukuru sana kwa kazi nzuri mliyoifanya Mwenyekiti wetu na Wajumbe wote ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mpaka Kamati ya Bajeti kufikia kufanyakazi yake vizuri na ninyi mmefanya kazi kubwa sana, kila Mjumbe wa Kamati ya Kisekta mmefanya kazi yenu vizuri sana na mawazo yenu ndiyo yaliyopelekea Kamati yetu ya Bajeti kuweza kusimamia hoja kadhaa zilizotoka kwenye Kamati zenu na sasa alipokuja Mheshimiwa Waziri na ile Bajeti ya Ujumla au Bajeti Kuu ya Serikali ameweza kuyachukua mawazo yenu mengi sana. Kwa hiyo, ninawapongeza sana

Wabunge wote kwa kushiriki kwenye zoezi hili kikamilifu kabisa na kwa kweli pongezi nyingi sana kwenu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, niliwashukuru hapa wasaidizi wangu lakini pia nichukue fursa hii kuwashukuru sana wasaidizi wangu Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa zoezi zima hili safari ilikuwa ndefu lakini umeweza kulisimamia Bunge vizuri nakushukuru sana. Mwenyekiti Mheshimiwa Najma Giga ahsante sana, kwa kazi nzuri ya usaidizi wa kusimama hapa mbele. Tunae pia Mwenyekiti Mheshimiwa David Kihenzile ahsante sana, kwa usaidizi mzuri mliotoa mpaka tunafikia sehemu hii. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa ujumla pia niwashukuru sana Serikali, Mawaziri wa Kisekta mmefanya kazi kubwa sana kwa kushirikiana na Wabunge, mmeyasikiliza mawazo yao, maoni yao ambayo baadaye mkayapeleka sasa yakaweza kufikia kwenye Bajeti Kuu ambayo ikaletwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango. Tunawashukuru sana kwa ushirikiano mlioonesha katika Bunge hili na nyinyi mmeona dhahiri kwamba Wabunge wamefurahi kwamba mawazo yao mmeyasikiliza. Tunawapongeza na kuwashukuru sana kwa usikivu huo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nafahamu yako baadhi ya mambo si mengi kwa bajeti hii kwa kweli si mengi lakini yako baadhi ambayo Serikali hamkuweza kukubaliana na Wabunge kwenye ngazi za Kisekta, lakini pia hata ngazi ya Bajeti Kuu kwa maana ya Kamati yetu ya Bajeti imeeleza mambo hayo kadhaa kwenye taarifa yake. Kwa namna ambavyo mmetoa ushirikiano mkubwa nataka kuamini kwamba yale ambayo hamjaweza kuyafanyia kazi katika bajeti hii ya 2022/2023 basi mmeyachukua yale ambayo wameyasema na mnayafanyia kazi, kwa maana ya kwamba tutakapokuja na *Inshallah* Mwenyezi Mungu atuweke mtakapokuja mwakani Serikali mtakuwa hayo mmeyatazama kwa mapana yake, mmeyafanyia utafiti na

wataalam wenu waweze kuona namna ambavyo mawazo ya Waheshimiwa Wabunge yanafanyiwa kazi hata yale ambayo hayakuweza kuingia katika bajeti hii ambayo tumeishaipitisha. Kwa hiyo, tunawatakia kila la kheri katika kuyafuatilia hayo ambayo Kamati imesema ambayo hamjaweza kuyafanya, lakini pia kwa ujumla wake utekelezaji wa bajeti yote ambayo Bunge imeipitisha tunawatakiwa kila la kheri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia nichukue fursa hii kwa sababu tunafahamu sisi sote kwamba Serikali kusikiliza mawazo ya Wabunge kama alivyosema Mheshimiwa Waziri hapa ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais kwa hiyo, tunamshukuru na yeye Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa kuonesha utayari wa kuwasikiliza Wabunge kama Wawakilishi wa wananchi mawazo yao na kuweza kuyafanyia kazi na kuona ni mambo ya msingi kabisa ambayo yanaweza kuboresha bajeti ya Serikali lakini kuboresha utendaji wake katika kuhakikisha inatekeleza zile ahadi ambazo ilizitoa kwa wananchi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunawatakia kila la kheri na tunaamini yale ambayo mmetuletea na sisi tumewapa ushauri na tumeyapitisha, mtaendelea kuyafanyia kazi na tunawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa bajeti hii mara Mheshimiwa Rais atakapopitisha Sheria hii kwa maana ya kuweka saini yake na ninyi kuanza utekelezaji tarehe Mosi Julai, tunawatakia kila lililo la kheri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge kwa kusema machache hayo naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 6.45 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 29 Juni, 2022 Saa Tatu Asubuhi)*